# Nipashe

Jumamosi Desemba 7, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580095

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

CEFA




## Utafiti waonyesha watu wengi kula nyama, mboga isiyo salama

UKURASA 3

# Laini milioni 29 bado kusajiliwa

**WENGI** hatarini kufungiwa mawasiliano, waliosajiliwa hadi sasa ni milioni 19...*Endelea ukurasa wa 2*



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Amina Lumuli na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Mhandisi Dk. John Ndunguru, wakipeperusha bendera jijini Dar es Salaam jana, kuzindua safari ya treni ya abiria ya Dar - Moshi mkoani Kilimanjaro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## WATOTO 64 FAMILIA DUNI WAFANYIWA UPASUAJI

UKURASA 3

## Taarifa ya DC yagomewa CCM

UKURASA 2




Scan Hapa

Pakua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store


**MICHEZO** SIMBA KUANDIKA REKODI MPYA LEO UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Laini milioni 29 bado kusajiliwa

**Waandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku 25 za usajili wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole, hadi sasa ambazo hazijasajiliwa ni milioni 28.7.

Mkuu wa Huduma za Masoko wa kampuni ya Tigo, William Mpinga, alisema hayo jana wakati akizungumza kwa niaba ya kampuni za mawasiliano nchini katika warsha kwa watumiaji mashuhuri wa mitandao ya kijamii kuhusu usajili huo.

Mpinga alisema laini ambazo zimesajiliwa hadi sasa kwa alama za vidole ni milioni 18.8.

"Hali halisi ya usajili wa laini za simu kwa alama za vidole mpaka sasa takwimu zinaonyesha zilizosajiliwa ni milioni 18.8 na ambazo bado hazijasajiliwa ni milioni 28.7.

"Tukiendelea na kasi hii tuliyo nayo huku muda uliobaki ni mfupi, laini ambazo hazijasajiliwa zinaweza zikawa milioni 16 sawa na asilimia 60.

"Tumewaita leo kwa sababu mitandao yenu ya kijamii ina nguvu ya kufikisha ujumbe, mtusaidie kuhamasisha usajili kwa watumiaji wa mitandao yenu ili watu milioni 20 wanaoitumia namba yao isishuke na kufikia milioni 12 kama hawataitikia wito huu kabla ya Desemba 31," alisema.

Alisema endapo watu milioni 16 hawatajisajili kwa alama za vidole watakuwa nje ya huduma kwa sababu laini zao zitafungiwa," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Emmanuel Manasseh, kwa upande wake alisema wamefanya warsha hiyo lengo likiwa ni kuhamasisha usajili huo kwa muda mchache uliobaki ambao mwisho ni Desemba 31.

"Usajili huu una madhumuni ya kuwalinda watumiaji wa huduma dhidi ya matumizi mabaya, kuwawezesha kutambuliwa na kuwawezesha watoa huduma kuwatambua wateja wao," alisema.

Dk. Manasseh alisema usajili huo wa alama za vidole umepunguza lile tatizo la 'Ile pesa nitumie

INAENDELEA UK. 8

# Taarifa ya DC yakataliwa CCM

**Na Mwandishi Wetu,** IGUNGA

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) wilayani Igunga mkoani Tabora kimekataa kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za serikali katika wilaya hiyo, kikieleza kuwa taarifa iliyowasilishwa imepitwa na wakati.

Imedaiwa kuwa taarifa hiyo iliyowasilishwa juzi kwa Halmashauri Kuu ya chama hicho wilayani humo na Mkuu wa Wilaya hiyo, John Mwaipopo, ni ya Julai hadi Desemba mwaka jana badala ya Julai hadi Desemba mwaka huu. Akitoa tamko hilo katika kikao hicho cha halmashauri kuu ya CCM wilaya, Mwenyekiti wa CCM wilayani humo, Regina Thadeo, alidai taarifa hiyo wamekataa kuipokea kwa imepitwa na wakati.

Alidai taarifa iliyowasilishwa katika kikao hicho ni ya utekelezaji wa shughuli za serikali kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2018 na sasa ni mwishoni mwa mwaka 2019, hivyo hawawezi kuipokea na wanaona ni dharau kwa chama. Aliongeza kuwa Halmashauri Kuu ya CCM wilaya ilimwelekeza mkuu wa wilaya huyo kuandaa upya taarifa ya utekelezaji wa shughuli za serikali katika wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Igunga, Mwaipopo, akizungumza na waandishi wa habari, alikiri kukataliwa kwa tarifa yake, lakini hakutaka kufafanua zaidi sababu za kupeleka taarifa iliyopitwa na wakati.



Naibu Balozi wa Saudi Arabia hapa nchini, Abdulaziz Hamad Alasim (mwenye kilemba chekundu), akibadilishana mawazo na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, baada ya kukutana na timu ya madaktari bingwa wa moyo kutoka Taasisi ya King Salman Humanitarian Aid and Relief Centre ya Saudia, iliyomaliza kambi ya upasuaji wa moyo, katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), jijini Dar es Salaam jana. Katika kambi hiyo, taasisi ya King Salman na Albalsam International zimefanikiwa kufanya upasuaji wenye mafanikio kwa wagonjwa 64. **PICHA: JOHN BADI**

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA(TALGWU)**

**TANGAZO LA UCHAGUZI MDOGO**

Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) kinataraji kufanya Mkutano Mkuu wa kazi wa miaka miwili na nusu ambapo pamoja na mambo mengine Mkutano huo utafanya Uchaguzi mdogo kujaza nafasi wazi za Uongozi katika Chama.

Uchaguzi unatarajiwa kufanyika tarehe 19 Desemba 2019 katika ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Royal Village Jijini Dodoma saa 03:00 Asubuhi.

Nafasi zitakazojazwa ni:
1. Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake Taifa
2. Mjumbe wa Mkutano Mkuu TUCTA - nafasi 8
3. Mjumbe wa Baraza Kuu TUCTA - nafasi 1
4. Mjumbe wa Kamati ya Ushauri Wanawake Taifa toka Halmashauri za Wilaya - nafasi 2

**Imetolewa na**

..............................
**Rashid M. Mtima**
**Katibu mkuu - TALGWU**

# JPM akerwa mvutano upanuzi wa hospitali

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ameonyesha kukerwa na mvutano wa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato mkoani Geita ambao wametumia muda mwingi kubishana kuhusu upanuzi wa majengo ya hospitali ya Chato licha ya Sh. Bilioni moja kutolewa.

Kutokana na mvutano huo, ameagiza upanuzi wa hospitali hiyo ufanyike mara moja kwa kuwa fedha zipo.

Rais Magufuli alitoa maagizo hayo jana baada ya kutembelea hospitalini hapo na kuwapa pole wagonjwa akiwamo Mzee Zephania Kanoge ambaye ndiye aliyemhamasisha kuingia katika siasa mwaka 1995.

"Serikali haiwezi kuvumilia kuona watu wakipata shida kwa uzembe wa viongozi wachache wa walmashauri. Viongozi wa halmashauri hii hakikisheni mnaanza mara moja upanuzi wa majengo haya kwa kuwa serikali imeshatoa fedha za ujenzi tangu mwezi Julai mwaka huu," alisema kupitia taarifa iliyotolewa na Ikulu.

Rais Magufuli alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Eliud Mwaiteleke, kuhakikisha ujenzi wa majengo hayo unafanyika na kwa gharama zinazostahili.

Pia amemtaka Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Ligobeth Kalisa, kuhakikisha mashine ya X-Ray inafanya kazi muda wote na wananchi wanapatiwa huduma kwa wakati.

"Si sawa kwa Hospitali ya Wilaya kukosa huduma za X- Ray eti kwa sababu hakuna mikanda ya kupigia picha," alisema.

Kuhusu historia ya mzee Kanoge, taarifa hiyo ya Ikulu ilisema yeye na mwenzake Constantine Misungwi (sasa marehemu), walimfuata Rais Magufuli mara mbili jijini Mwanza alikokuwa akifanya kazi katika Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza wakimtaka agombee ubunge.

"Licha ya kukataa, wazee hao waling'ang'ania hadi alipokubali na wakabeba jukumu la kumfanyia kampeni kwa kutumia pikipiki hadi aliposhinda uchaguzi," ilisema taarifa hiyo.

Baada ya kumjulia hali, Rais Magufuli alimshukuru mzee hiyo kwa mchango wake mkubwa katika maisha yake ya siasa na amemuombea apone haraka ili aweze kurejea nyumbani na kuungana na familia yake.

Akiwa hospitalini hapo, Rais Magufuli aliwaona wagonjwa wengine pamoja na wanawake na watoto waliofika kupata chanjo na kuwahakikishia kuwa serikali imeanza kuchukua hatua madhubuti za kuboresha huduma za afya.

**HABARI KITAIFA**

# Utafiti: Watu wengi wanakula nyama, mboga isiyo salama

**Na Juster Prudence**

RIPOTI ya walaji wa nyama na mboga nchini imeonyesha kuwa walaji wengi hawana uelewa wa usalama wa nyama, jambo linalowafanya kununua kienyeji bila kujali afya zao.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Kulinda Wanyama Duniani iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam, watumiaji wa nyama hawajui jinsi gani wanyama wanatakiwa kutunzwa kabla ya kufanywa kitoweo .

Ripoti hiyo ilionyesha asilimia 37.2 ya watumiaji kutoka nchini hawatilii maanani suala la nyama kuchafuliwa na kemikali ambazo zinaweza kuwa hatari kwao.

Aidha, alisema asilimia 54.37 hawachukulii maanani ustawi wa wanyama huku asilimia 60.7 na 56.8 wakiwa hawajui kabisa faida za utunzaji au ustawi mzuri wa wanyama katika ukuaji wanyama.

Meneja wa Kampeni ya Utunzaji wa Wanyama Duniani, Dk. Victor Yamo, alisema utafiti uliofanyika ulionyesha kuwa Watanzania wengi wako tayari kulipa zaidi katika ununuzi wa vyakula hivyo ikiwamo nyama kama watahakikishiwa ubora, kama vile kutokuwa na kemikali au viambata vya sumu vya aina yoyote.

Kwa mujibu wa meneja huyo, asilimia 89.9 ya watumiaji hununua nyama na vyakula vinavyotengenezwa kwa nyama katika migahawa na maduka mbalimbali yanayojihusisha na uuzaji wa vyakula nchini.

Pia alisema tathmini hiyo inaonesha kuwa asilimia 38.2 ya watumiaji hao wangeweza kununua zaidi kama kungekuwa na mazingira mazuri ya utengenezaji wa vyakula hivyo.

Dk. Yamo alisema ipo haja ya kutoa elimu kwa watumiaji wote pamoja na wauzaji wa vyakula juu ya ubora wa nyama tutakayopata kama tutazingatia ustawi wa wanyama hao ikiwa ni pamoja na mazingira wanayotegemea kwa ajili ya ukuaji.

Alibainisha kuwa elimu pekee haitatosha kubadili taswira hiyo kama hakutakuwa na sheria maalum zinazolinda ustawi wa wanyama na usalama wa vyakula.

Mtaalamu huyo alifafanua kuwa lengo la kampeni hiyo siyo tu kuwalinda watumiaji bali kuhakikisha Tanzania inafikia viwango vya kimataifa katika ubora wa vyakula.

Ripoti hiyo pia imeonyesha kuwa asilimia 53.3 ya Watanzania wanatumia dawa za kuua wadudu katika mashamba yao ili kupunguza upatikanaji mbovu wa mazao huku asilimia 79.4 ya watumiaji wakiwa na imani ya kwamba dawa za kuua wadudu kwenye mazao huchangia kuongeza kemikali katika mazao.

Aidha, alisema asilimia 87.8 ya watumiaji wakielezea kuona madhara yanayosababishwa na ustawi mbaya wa wanyama ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa nyama isiyo na ubora huku asilimia 61.8 ya watumiaji wamesema wako tayari kuongeza malipo kwa ajili ya nyama itakayotengenezwa kwa viwango.

# Watoto 64 familia duni wafanyiwa upasuaji

**Na Juster Prudence**

WATOTO 64 kutoka familia maskini wamefanyiwa upasuaji wa moyo wakati wa kambi maalum ya madaktari 19 kutoka taasisi ya King Salman nchini Saudi Arabia.

Upasuaji huo umefanyika kwa ushirikiano na jopo la madaktari wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Profesa Mohamed Janabi, alisema madaktari hao waliweka kambi nchini kwa ajili ya kuwezesha upasuaji huo kwa watoto waliokuwa wamelazwa kusubiri matibabu.

Alisema pamoja na watoto hao kufanyiwa upasuaji, bado kuna zaidi ya watoto 500 wanaohitaji kufanyiwa upasuaji na kwamba unaendelea hadi Desemba 30, mwaka huu kwa watoto 50 kutoka nchini na wawili wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo, wagonjwa 300,836 wamepata huduma mbalimbali kati yao 1,537 walifanyiwa upasuaji.

Naye Balozi Mdogo wa Saudi Arabia nchini, Abdulaziz Hamad Alasim, alisema nchi hizo zina uhusiano mzuri ambao umesaidia kutoa msaada wa madaktari ili kuwasaidia Watanzania wengi kujali hali zao.

"Kama ubalozi tutahamasisha madaktari kutoka nchini Saudi Arabia ili siku nyingine waje wengi zaidi ya waliopo

INAENDELEA UK. 8


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la upimaji wa viwanja limekamilika na kuanzia **TAREHE 3/12/2019** viwanja vitaanza kuuzwa kila siku za Jumatatu hadi Ijumaa katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 2 Asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.

**Viwanja vinavyouzwa ni katika maeneo ya:**

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| NALA (Karibu na Chuo cha IFM na Kituo cha kupaki Malori) | • Makazi 4,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| CHAHWA (Karibu na Ikulu) | • Makazi 3,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| Mahoma Makulu (Nyuma ya Mji wa Serikali) | • Makazi 3,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| KIKOMBO (Karibu na Bandari kavu na Makao Makuu ya Ulinzi ya Taifa) | • Makazi 2,000/=<br>• Makazi na Biashara 3,500/= |
| MTUMBA (Karibu na Mji wa Serikali na Ikulu) | • ZONE I Makazi 8,000/= Makazi na Biashara 8,500/=<br>• ZONE II Makazi 6,000/= Makazi na Biashara 7,500/=<br>• ZONE III Makazi 3,000/= Makazi na Biashara 5,500/= |

**NB: Malipo yote yafanyike ndani ya Siku 90 baada ya kupata hati ya madai.**

***Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba 0714 785513.***

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

215542002

## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## MNADA WA UUZAJI WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la uuzaji wa Viwanja kwa njia ya Mnada litafanyika tarehe **14 Disemba, 2019** siku ya Jumamosi. Mnada utafanyika katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 4:00 Asubuhi.

Viwanja vinavyouzwa ni Maeneo ya:

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| IYUMBU (New Town Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Viwanda Vidogo |
| NALA (Industrial Area) | • Viwanja vya Viwanda vya aina mbalimbali |
| NJEDENGWA (Investment Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara |
| NZUGUNI (Jirani na Uwanja wa Mpira, Soko Kuu na Stendi kuu mpya ya mabasi) | • Viwanja vya Hoteli<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Maduka makubwa (Shopping Malls) |

**NB**:

- Asilimia 50 ya Malipo italipwa siku ya Mnada
- Asilimia 50 inayobaki italipwa ndani ya siku 14 baada ya Mnada.

Tangazo hili limetolewa na:
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

# Waziri atishia kufuta wakala wa mbegu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ametishia kuifuta Bodi ya Wakala wa Mbegu (ASA), endapo itashindwa kusimamia majukumu yake ipasavyo. Aidha, ametaka wakala huo kuzalisha mbegu za kilimo zipatazo tani 5,000 katika msimu wa kilimo wa mwaka 2019/20.

Akizungumza jana na watumishi wa taasisi hiyo baada ya kutembelea mkoani Morogoro, alisema pia hatua zitachukuliwa dhidi ya Mtendaji Mkuu wa Wakala.

Amesema pamoja na ASA kuongeza eneo la uzalishaji wa mbegu kutoka hekta 9,890 hadi 10,115.2 bado uzalishaji ni mdogo kwa kuwa inazalisha tani 1,440 pekee huku zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania wanaojihusisha na kilimo wakiwa na uhitaji wa mbegu. Waziri Hasunga alisema matrekta matatu mapya yaliyonunuliwa na ASA pamoja na zana zake kama vile Boom Spayer, majembe matatu mapya na planter tatu mapya yanapaswa kutumika ipasavyo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora.

"Sisi kama nchi tunahitaji tani 100,086 za mbegu na mpaka sasa hivi uwezo wetu wa kuzalisha ndani na kuagiza nje hauzidi tani 57,000 sasa mahitaji ni makubwa watu wanataka mbegu bora lakini uzalishaji bado upo chini," amesisitiza. Waziri Hasunga alisema mbegu bora ndio msingi na muhimili wa kilimo hivyo, ili kubadilisha kilimo kutoka kujikimu na kuwa kilimo chenye tija na cha kibiashara ni lazima kuwa na uzalishaji mkubwa wa ndani ya nchi.

Aliongeza kuwa serikali itaiwezesha ASA kuongeza vituo vya usambazaji wa mbegu kutoka vitano ambavyo vinatumika sasa mpaka kuwa vituo 10, ili kuwarahisishia wakulima kupata mbegu katika maeneo yao. Kadhalika, waziri Hasunga alimtaka Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu (ASA) kuhakikisha kuwa anatatua changamoto alizozibainisha kwenye taarifa yake ikiwemo ukosefu wa mtaji wa kutosha, kutokuwa na hifadhi ya mbegu ya Taifa, ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji, upungufu wa vitendea kazi na uhaba wa vituo vya kusambaza mbegu.

Changamoto zingine ni upungufu wa magari ya kusambaza mbegu, uchakavu wa mitambo ya kuchakata mbegu, na upungufu na uchakavu wa maghala ya kuhifadhi mbegu.




Mfanyakazi wa kampuni ya udalali (kulia), akiwa amemkamata mwendesha bodaboda katika eneo la Lumumba, baada ya kuingia katika Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam jana, bila ya kuwa na kibali maalum. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Pasipoti ya Bulaya yadaiwa mahakamani

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo tisa wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), umesisitiza mahakamani unataka hati ya kusafiria ya Mbunge wa Jimbo la Bunda, Ester Bulaya, kupelekwa kwa ajili ya kumfanyia mahojiano.

Bulaya ambaye ni mshtakiwa wa tisa katika kesi hiyo, alidai kuwa siku ya tukio alikaribishwa kusalimia wananchi jukwaani, aliondoka eneo hilo kwenda Mbweni kujiandaa na safari ya kumsindikiza rafiki yake Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, kwenye matibabu Afrika ya Kusini.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Mushi, ilikubali kuahirisha kesi mpaka Desemba 19, mwaka huu, mbunge huyo atakapowasilisha hati yake ya kusafiria na kuendelea kuhojiwa na Jamhuri.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na wakurugenzi wasaidizi wa mashtaka, Faraja Nchimbi na Pendo Makondo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Jaqline Nyantori.

Akihojiwa na Wankyo, shahidi huyo alidai kuwa Februari 16, 2018 alikuwapo katika viunga vya Buibui na kwamba mshereheshaji wa mkutano wa kufunga kampeni, Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, alimkaribisha jukwaani, alipanda na kuwasalimia wananchi.

Hata hivyo, alidai ilipofika saa 11 aliongozana na Mdee kwenda nyumbani Mbweni na kwa sababu alimweleza anaumwa na alilazimika kusafiri naye kwenda Afrika Kusini kwa matibabu.

Akiongozwa na Wakili wa utetezi, Peter Kibatala, shahidi huyo alidai kuwa kati ya Februari Mosi na 11, alikuwa kwenye vikao vya Bunge Dodoma, Februari 11 na 15, alikwenda jimboni Bunda na alifika jijini Dar es Salaam Februari 16, 2018 saa 9:30 alasiri kwa ajili ya kuhudhuria kufunga kampeni.

"Mdee ni mbunge mwenzangu na pia ni, rafiki yangu alinieleza kwamba anajisikia vibaya anaumwa tukiondoka wote saa 11 na dakika zake kwenda Mbweni na nililazimika kumsindikiza hospitali ya St. Parot, nchini Afrika Kusini baada ya wiki mbili au tatu tulirejea, lakini Mdee alikamatwa Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere," alidai na kuongeza:

"Wakati wote wa matibabu ubalozi wetu Afrika Kusini haukuwahi kutufahamisha kama tunatafutwa, niliporejea nchini baada ya wiki mbili nilipigiwa simu nikiwa jimboni Bunda kwamba natafutwa na polisi," alidai Bulaya.

Alidai kuwa kuhusu madai ya hati ya mashtaka kueleza kwamba aliwachochea wananchi wa Kinondoni kuandamana, si kweli kwa sababu hakuna shahidi wa Jamhuri aliyethibitisha kama watu walioandamana ni wakazi wa eneo hilo.

Kesi hiyo itaendelea Desemba 19, mwaka huu, upande wa Jamhuri utakapoendelea kumhoji mshtakiwa Bulaya.

Mbali na Bulaya na Mdee washtakiwa wengine ni Mwenyekiti wa Chadema Freeman Mbowe, Katibu Mkuu Taifa, Dk. Vicent Mashinji, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar Salum Mwalimu, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche na Mbunge wa Kibamba John Mnyika.

Pia wamo Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji jinai kati ya Februari Mosi na 16, 2018, jijini Dar es Salaam.




## HABARI KITAIFA

# RAS ahofia wanafunzi kupewa ujauzito kabla ya kuanza shule

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, ameingiwa na hofu ya baadhi ya wanafunzi wa kike ambao wamefaulu mkoani hapa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, kushindwa kuripoti shuleni kutokana na kupewa ujauzito.

Mkoa wa Shinyanga umeendelea kukabiliwa na tatizo kubwa la wanafunzi kupewa ujauzito. Mwaka jana wanafunzi 69 walipewa ujauzito na mwaka huu mpaka sasa taarifa zilizopo ni mimba 120.

Msovela alibainisha hayo jana kwenye kikao cha uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani kuwa kutokana na mkoa kukabiliwa na tatizo hilo, ameingiwa na hofu kuwa huenda baadhi ya wanafunzi wa kike wasiripoti shuleni kwa sababu hizo.

"Shinyanga ni kati ya mikoa 13 nchini ambayo wanafunzi wake waliofaulu wote wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza. Kama mlivyomsikia jana (juzi) kwenye vyombo vya habari, Waziri (wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Selemani) Jafo akitangaza matokeo hayo, hofu yangu kubwa sijui kama wanafunzi wote wa kike wataripoti shuleni kama hawatakutwa na ujauzito," alisema Msovela.

"Natoa maagizo kwa maofisa elimu ngazi zote, mfuatilie wanafunzi wote waripoti shuleni. Yule ambaye atakutwa amepewa ujauzito kuchueni hatua na kumfuatilia yule ambaye amempatia na kumpeleka kwenye vyombo vya sheria apate kuchukuliwa hatua kali za kisheria ili liwe fundisho kwa watu wengine,"aliongeza.

Akitangaza wanafunzi waliochanguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani mkoani hapa. Msovela alisema wanafunzi 23,634, wakiwamo wavulana 11,280 na wasichana 12,354 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Wanafunzi hao ni kati ya 30,393 wakiwamo wavulana 14,322 na wasichana 16,071 waliofanya mitihani hiyo. Waliofeli ni wanafunzi 6,759 ambao niwavulana 3,042 na wasichana 3,717.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba, alisema ili tatizo la mimba za wanafunzi likome mkoani hapa, ni lazima kila mtu atekeleze majukumu yake, wakiwamo walimu wakuu, watendaji wa vijiji, wazazi, polisi, madaktari, mahakimu, kwa kuacha kuharibu ushahidi ili watuhumiwa wafungwe jela.

Kwa upande wake, Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Mohamed Kahundi, alielezea kusikitishwa na kitendo cha wazazi kuacha kuwapeleka watoto wao wa kike kuishi kwenye shule ambazo zina bweni na kuwapangia mitaani maarufu kama 'mageto', hali ambayo alisema imekuwa ikichochea tatizo la mimba za wanafunzi.

# TCAA yakiri upungufu marubani wazawa

**Na Beatrice Moses**

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imesema nchi inakabiliwa na uhaba wa marubani wazawa na wataalam wa mitambo ya ndege.

Aidha, katika utatuzi endelevu, wameanzisha mashindano ya uandishi wa insha maalum za masuala ya ndege kwa wanafunzi.

Hayo yalibainisha jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Vallery Chamlungu, wakati wa hafla ya kuwatunza washindi wa insha kuhusu 'Mchango wa Shirika la Ndege la Taifa katika Uchumi wa Nchi'.

Alisema mara kadhaa TCAA inatangaza nafasi za kazi lakini linarudiwa mara nyingi bila kupata wataalam na marubani husika, jambo ambalo linaonyesha kwenye sekta hiyo kuna uhaba wa wanataaluma hao.

Chamlungu alisema shindano hilo la kwanza liliwahusu wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wenye umri wa miaka kati ya 10 na 13, na kwamba litakuwa endelevu.

"Hii ilitokana na ukweli kuwa, tunatambua umuhimu wa kukuza uelewa wa vijana kuhusu sekta kuanzia ngazi ya chini, ili kuwajengea msingi mzuri kuhusu sekta hii," alisema Chamlungu.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kupitia insha hizo, wamebaini kuwa vijana wengi wana ari ya kujifunza kuhusu sekta ya usafiri wa anga na kwamba mamlaka hiyo itaendelea kujenga mazingira ya kuwafikia.

"Tayari kupitia baraza la watumiaji wa huduma za usafiri wa anga, limeanzisha klabu za usafiri wa anga katika sekondari za Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Mtwara na tunaendelea kwenye mikoa mingine," alisema.

Jaji wa shindano hilo, Abubakar Noor, ambaye ni mkufunzi wa mafunzo ya uhandisi wa ndege kutoka Chuo cha Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC), alisema walipokea isha 100 kutoka kwa wananchi katika mikoa mbalimbali nchini.

Alisema pamoja na kupokea insha hizo wakaweka utaratibu wa kupata washindi watano baadha ya mchujo, walitakiwa kuwasilisha maandiko yao katika hafla hiyo, ili kubaini uwezo wa uelewa wao.

Albert Dida aliibuka kuwa mshindi wa kwanza na kuzawadiwa kompyuta mpakato kwa kuwashinda Hazeifa Amirali, Alpha Mbise, Maureen Silayo na Yvonne Lyaruu.

Hafla hiyo ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga Dunia (ICAD) ambayo inakwenda sanjari na maadhimisho ya miaka 75 tangu kuanzishwa kwa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO).


**CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)**
(Tanzania Teachers' Union – TTU)

P.O. Box 3077 DODOMA
Cable: WALIMU DODOMA
E-mail: info@ttu.or.tz
Fax: 255 262323452
Telephone: 255 262323451

**INVITATION FOR PRE QUALIFICATION FOR PROPOSED CONSTRUCTION OF OFFICE BUILDING AT CHATO**

**6th December, 2019**

1. Tanzania Teachers Union (TTU) has set aside funds towards the cost of the construction of its district office at Chato and it intends to apply part of the proceeds of this funds to cover eligible payments under the contract for office building construction. Tanzania Teachers Union now intends to pre-qualify Applicants for construction of office building at Chato, Geita. It is expected that invitations to tender will be made in January, 2020.

2. Pre-qualification will be conducted through the procedures specified in Regulation 119 of the Public Procurement (Regulations– Government Notice 446 of 2013, and is open to all Applicants as defined in the Regulations.

3. Tanzania Teachers Union intends to pre-qualify contractors registered in Class Five (5) and above in Building Category for the proposed construction of an office building at Chato.

4. Interested applicants may submit applications at the office of General Secretary, TANZANIA TEACHERS UNION, CWT Building Jamhuri Street, Dodoma municipal in Dodoma on or before 20th December, 2019.

5. All applications in one original plus two copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below on or before 1400 hours 20th December, 2019. Applications will be opened promptly thereafter before the Tender board on the day of tender opening.

6. The outer cover containing the applications shall be properly marked **"GENERAL SECRETARY, TANZANIA TEACHERS UNION (TTU), P.O. BOX 3077 DODOMA**

7. Tender board team will evaluate using on but not limited to the following criteria's;
   i. Company Experience
   ii. Company Organization
   iii. Structure i.e management processes, operational procedures, & turnover.
   iv. Quality
   v. Safety
   vi. Senior Management
   vii. experience
   viii. Current Projects/Backlog
   ix. number, size, and location of projects i.e percent of capacity being utilized, status and expected completion period
   x. Financial Strength

8. Late applications, portion of applications, electronic applications, and applications not received, applications not opened and not read out in tender board at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

Mwl. Deus G Seif
GENERAL SECRETARY
TANZANIA TEACHERS UNION

GENERAL SECRETARY
TANZANIA TEACHERS' UNION (TTU)
DODOMA - HEADQUATERS

215547302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kili Stars, Zanzibar Heroes fanyeni kweli Chalenji

**KIPENGA** cha kufunguliwa kwa michuano mikongwe Afrika [Kombe la Chalenji] mwaka huu kinatarajiwa kuanza kupulizwa leo kwa wenyeji, timu ya soka ya Taifa ya Uganda (Cranes), kuwakaribisha Burundi katika mechi ya ufunguzi ya kinyang'anyiro hicho itakayopigwa kwenye Uwanja wa Namboole jijini Kampala, Uganda majira ya saa 10 jioni.

Michuano hiyo ya Cecafa Chalenji inaheshima yake Afrika kwani ndiyo mikongwe zaidi ya soka barani humu kutokana na kuanza mwaka 1926 ikijulikana kama Kombe la Gossage hadi mwaka 1966, ilipobadilishwa na kuwa Kombe la Mataifa ya Afrika Mashariki na Kati kabla ya 1971 kubadilishwa na kuwa Cecafa Challenge.

Mechi hiyo Uganda dhidi ya Burundi inatarajiwa kutanguliwa na mchezo mwingine kati ya Djibouti dhidi ya Somalia, utakaochezwa kwenye uwanja huo huo, kuanzia majira ya saa nane mchana.

Hata hivyo, macho na masikio ya Watanzania yanatarajiwa kuelekezwa zaidi uwanjani kesho watakati timu zao mbili za Taifa, Kilimanjaro Stars ya Tanzania Bara na Zanzibar Heroes ya Tanzania Visiwani, zitakaposhuka dimbani kwa nyakati tofauti.

Kilimanjaro Stars itashuka dimbani kupepetana na mabingwa watetezi, Harambee Stars ya Kenya wakati Zanzibar Heroes itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Sudan.

Katika michuano hiyo ambayo washindi wawili kutoka katika kila kundi watatinga nusu fainali, Kundi A linaundwa na wenyeji Uganda, Burundi, Eritrea, Somalia na Djibouti wakati Kundi B mbali ya Kilimanjaro Stars na Zanzibar Heroes, pia zimo Kenya na Sudan.

Mbali na kuwania ubingwa, michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), inatarajiwa kutoa nafasi nzuri kwa timu za ukanda huu zilizofuzu Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa ndani (CHAN), kujiandaa na mashindano hayo yatakayofanyika Aprili mwakani.

Hivyo ni matarajio yetu kuona Kili Stars, mabingwa wa 1975, 1994 na 2010 ama Zanzibar Heroes walioutwaa ubingwa huo mwaka 1995, timu mojawapo kati ya hizo ikirejea na taji hilo linaloshikiliwa na Harambee Stars kwa sasa.

Tunatambua haitakuwa michuano rahisi hasa kwa kuzingatia Harambee Stars, watataka kulitetea taji hilo, lakini pia wakipania kulipa kisasi kwa Tanzania ambayo iliwatoa kwenye michuano ya kuwani kufuzu CHAN Agosti mwaka huu.

Aidha, vita ya kuutwaa ubingwa huo haipo kwa Kenya na timu hizo za Tanzania pekee, bali pia tunatambua uwapo wa timu imara ya Uganda kutoka Kundi A, ambo ni mabingwa wa kihistoria wa michuano hiyo tangu mwaka 1971, wakiwa wameutwaa mara 14, wakifuatiwa na Kenya mara saba na kisha Ethiopia ambayo imejitoa kutokana na kukabiliwa na ukata ikiwa imeubeba mara nne.


Lakini hilo halitutii hofu kwani tunaamini, Kilimanjaro Stars ikiwa chini ya Kocha Juma Mgunda itaandika historia mpya kwa kuifikia Ethiopia kwa kuutwaa ubingwa mara ya nne na kama hilo likishindikana, basi Hemed Morocco ataiongoza vema Zanzibar Heroes na kuokoa jahazi kwa kurejea na taji hilo nchini.

Mbali na matarajio hayo, lengo letu ni kuona wachezaji wa Kilimanjaro Stars na wale wa Zanzibar Heroes wakionyesha uwezo mkubwa uwanjani ili kutoa wigo mpana kwa Kocha wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije kuchagua nyota watakaounda kikosi chake.

Katika michuano hii ya Cecafa, Ndayiragije atakuwa nchini Uganda kama mshauri wa makocha wa timu hizo mbili za Tanzania, lakini pia akilenga kuangalia wachezaji watakaounda kikosi cha Taifa Stars, hivyo ni wakati wa kila mmoja atakayepata nafasi kuonyesha uwezo wake ili kumshawishi kocha huyo wa timu ya taifa.

Hivyo, wakati wachezaji wakitekeleza wajibu huo, mashabiki, wadau wa soka na Watanzania kwa ujumla, hawana budi kuungana nazo nchini Uganda kuzishangilia na wale watakaoshindwa dua na maombi yao ni muhimu sana ili timu hizo za Tanzania ziweze kufanya kweli na kurejea na taji hilo ambalo kwa mara ya mwisho kubaki hapa nchini ilikuwa mwaka 2010 lilipobebwa na Tanzania Bara wakati huo ikiwa chini ya kocha Mdenmark, Jan Poulsen na michuano hiyo ikifanyika jijini Dar es Salaam.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kweli ndio fimbo ya kukamata



Na Barnabas Maro

**KWELI** ni silaha nzuri maishani. Methali hii hutukumbusha umuhimu wa kusema kweli hata kama kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na wenzetu.

Mechi ya Jumatatu iliyopita kati ya Yanga ambayo sasa yaitwa 'Timu ya Wananchi,' na timu ya Manispaa ya Kinondoni (KMC) iliniwacha kwenye bumbuazi (mshangao mkubwa unaofanya mtu awe kimya na asijue la kufanya).

Pamoja na bumbuazi hilo, ningali najiuliza kama baadhi ya waamuzi wetu wa mchezo wa kandanda wanaelewa kanuni (sheria ndogo ndogo zilizoundwa kurahisisha utekelezaji wa sheria mama inayosimamia jambo fulani) zote za kuchezesha mchezo huo.

Napata hofu (hisia ya kuogopa) kusema kuwa mechi ile timu zilitoka 'sare kwa kufungana bao 1-1.' Binafsi, ingawa ni mwanachama wa Yanga tangu Desemba 2, 1966 kwa kadi namba 447 sikubaliani na sare ile. Kadi yangu ya nne inayotumika sasa imeandikwa: "Wajibu wa Mwanachama ni kuwa mkweli wakati wote na mwaminifu kwa Klabu." Natekeleza wajibu wangu ingawa najua kuna watakaonipinga.

Ilisemwa na wahenga kuwa "Kweli ndio fimbo ya kukamata." Maana yake kweli ni silaha nzuri maishani. Hii ni methali ya kutukumbusha umuhimu wa kuusema ukweli hata kama kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na wenzetu.

Kadhalika, walisema: "Kweli chungu si uongo mtamu." Maana yake ni heri kusema ukweli mchungu kuliko uongo mtamu. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuukabili ukweli ijapokuwa una uchungu kuliko kuushabikia uongo.

Kujitapa kuwa Yanga na KMC zilitoka sare kwa kufungana bao 1-1 si kweli bali tunajidanganya mchana kweupe. Kwa mtazamo wangu usio na shaka na ulio sahihi, Yanga ilifungwa 2-1 hivyo washindi ni KMC dhidi ya Yanga.

Najua kuna watakaoguna (kitendo cha kutoa sauti za ndanindani zinazoonesha kutoridhishwa na msimamo wangu), hata kubisha na kuniita 'msaliti.' Nimeeleza huko juu kuwa "Kweli chungu si uongo mtamu." Waseme watakavyo lakini msimamo wangu ni uleule: Yanga tulifungwa 2-1 na wale vijana wa KMC waliocheza kandanda lililowavutia watazamaji wanaojua kandanda lilivyo.

Kwa wale wanaotazamia ushindi tu hata kama timu haichezi vizuri, nawapa pole. Nawasikitikia kwani watu wa aina hiyo ndiwo waharibifu wa timu kwa kutojua ushindi unavyopatikana. Simo upande wao. Nilivyo ni kwamba hata timu zangu (Yanga au Taifa Stars) zikishindwa, lakini zilionesha mchezo mzuri, nitazisifu kwani kandanda ni mchezo wa bahati.

Timu yaweza kucheza vizuri sana lakini ikapoteza na kuwashangaza wengi. Bila kuficha wala kumunyamunya (kitendo cha kutikisa midomo kama mtu anayetaka kusema au kucheka), wallahi KMC walicheza mchezo mzuri unaoeleweka kuliko walivyokuwa wachezaji wa Yanga.

Mara nyingi juhudi zao zilizuiwa na walinzi wa Yanga ingawa waliweza kumiliki mpira tangu langoni mwao na kupiga hodi kwenye lango la Yanga, ila bahati haikuwa yao!

Ikumbukwe kuwa mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu msimu uliopita, Simba ilicheza vizuri mno dhidi ya Yanga, lakini ziltoka suluhu bila kufungana.

Yanga tulishangilia utadhani tulishinda! Mchezaji aliyeinyima Simba ushindi si mwingine bali ni aliyekuwa mlinda mlango wa Yanga ambaye sasa yupo Simba baada ya kuachwa na Yanga. 'Kosa' lake, kama naweza kusema hivyo, ni kipa huyo kudai haki zake yaani bakaa ya fedha za usajili wake Yanga na malimbikizo ya mishahara yake tu basi! Wewe ungekubali? Turudi nyuma.

KMC walionana vizuri kiasi cha wachezaji wao kupiga chenga za maudhi kuanzia mmoja mpaka wanne kuelekea goli la Yanga ila hawakuwa na bahati kama ilivyokuwa msimu uliopita Yanga ilivyoponea chupuchupu kufungwa na Simba mzunguko wa kwanza.

Turudi kwenye mchezo wa Yanga dhidi ya KMC. Katika hekaheka za kutaka kufunga, mchezaji wa KMC aliangushwa eneo la penalti kwenye goli la Yanga, lakini refa hakupuliza filimbi kuashiria penalti kuelekea Yanga! Tukio lile lilioneshwa na kurudiwa zaidi ya mara tatu na runinga ya Azam iliyorusha mchezo ule mubashara (moja kwa moja) na kuonekana mchezaji wa KMC akichezewa rafu ya wazi kwenye eneo la penalti. Refa 'akalifumbia macho' tukio lile!

Vuta hisia kama tukio la kunyimwa penalti wangefanyiwa Yanga pangekuwaje pale uwanjani? Wallahi mwamuzi na washika vibendera wake wangetoka uwanjani kwa ulinzi mkali wa Jeshi la Polisi.

Mpira uliomfikia mchezaji wa KMC naye kuchezewa vibaya nje ya eneo la penalti ndipo mwamuzi akapuliza filimbi ingawa mpira uliopigwa kuelekea Yanga haukuwa na madhara yoyote kwao.

Kwa kuwa haki ya mtu haipotei, zikiwa zimesalia dakika chache mchezo umalizike, KMC wakapata penalti na kupata bao la kusawazisha kuwa 1-1.

Kama si hivyo KMC ingelala kwa kufungwa bao 1-0. Kama penalti waliyonyimwa ingepigwa, huenda KMC wangetoka uwanjani vifua mbele kwa kuwafunga mabingwa wa kihistoria, Yanga mabao 2-1.

Anayebisha abishe tu lakini ukweli ndio huo. Hata kama kusema ukweli wangu nitanyang'anywa kadi, potelea mbali ninyang'anywe lakini nitabaki kuwa Yanga bila kadi kwani si wote wanaoipenda Yanga wana kadi za uanachama.

HABARI KITAIFA

# Wizara tatu kunusuru utalii Mafia

Na Lusungu Helela

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amesema kuna haja ya wizara tatu zinazohusika na usimamizi wa Kisiwa cha Mafia kukutana ili kufanya majadiliano kunusuru utalii katika kisiwa hicho.

Hatua hiyo inakuja baada ya malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali wa utalii kutokana na tozo ya dola 240 (sawa na Sh. 552,0000 za Kitanzania ) inayotozwa kwa kila mtalii na Mamlaka ya Hifadhi ya Bahari.

Tozo hiyo ni nje na mbali na tozo za utalii hali inayosababisha watalii wengi kushindwa kumudu gharama hizo.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na wadau wa utalii katika mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji.

Mkutano huo uliolenga kutatua changamoto wanazokabiliana nazo na uliwakutanisha mawaziri 13 wa wizara mbalimbali wakiongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki.

Kanyasu amesema tozo hiyo imekuwa kikwazo kwa watalii kwa vile kila mmoja anatakiwa kulipia kiasi hicho pasipo kujali ametembelea fukwe za bahari ili mradi tu kafika katika kisiwa hicho.

Akijibu baadhi ya malalamiko kutoka kwa wadau hao, Kanyasu alitaja wizara zinazotakiwa kukutana kuwa ni Mifugo na Uvuvi yenye dhamana na kisiwa hicho, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) inayosimamia uwekezaji na Maliasili na Utalii inayosimamia utalii.

Alisema licha ya kuwa Mafia ni miongoni mwa visiwa bora barani Afrika, kimekuwa kikipata idadi ndogo sana ya utalii kutokana na wengi kushindwa kutembelea huko kutokana na tozo kubwa inayotozwa na Mamlaka ya Bahari kwa watalii.

Kwa mujibu wa takwimu, kisiwa hicho kimekuwa kikipokea watalii 5,000 kwa mwaka na walio wengi wakiwa ni watalii wa ndani

Alisema kwa vile kisiwa hicho kimekuwa kikisimamiwa na zaidi ya wizara moja huku kila moja ikitekeleza jukumu lake, ni lazima wizara hizo zikutane ili kuona uwezekano wa kuwaviutia watalii wengi kutembelea kisiwa hicho.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, Zanzibar kila wiki imekuwa ikipokea ndege mbili za watalii wapatao 5,000 huku Mafia ikipata watalii 5,000 kwa mwaka kutokana na gharama kuwa kubwa.

Awali, mmiliki wa hoteli za utalii Mafia, Juma Awadhi, akichangia hoja katika mkutano huo, alisema hoteli zilizoko katika kisiwa hicho, zimekuwa zikikosa watalii, hivyo kulazimika kufanya biashara katika mazingira magumu.

"Mheshimiwa Waziri kuna siku hoteli zinakosa watalii kabisa, hakuna mgeni hata mmoja ilhali Mafia ni kisiwa bora barani Afrika," alisema.

Naye Janeth Kinala, mfanyabiashara wa mboga katika kisiwa hicho, alisema kutokana na ukubwa wa tozo hiyo, biashara yake imedumaa kwa kuwa soko lake kubwa lilikuwa wamiliki wa hoteli wanaonunua kwa ajili ya watalii.



Katapila la mkandarasi likiendelea na kazi ya ukarabati wa Barabara ya Sewa, eneo la Mikocheni Viwandani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Huduma Bandari ya Mwanza yaongozeka

Na Elizabeth Zaya, MWANZA

BANDARI ya Ziwa Victoria jijini Mwanza, imehudumia shehena tani 76,168.44 ya lengo tani 76,833 katika kipindi cha Julai hadi Novemba, mwaka huu.

Mapato yatokanayo na shughuli za kupakua shehena bandarini yameongezeka kutoka Sh. milioni 1,133.61 mwaka 2014/15 hadi kufikia Sh. milioni 1,422.19 mwaka 2018/19.

Hayo yameelezwa jana na Meneja wa Bandari hiyo, Morris Mchindiuza, wakati wa ziara ya waandishi wa habari kutembelea kujionea utendaji kazi wa bandari hiyo iliyoko chini ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Alitaja sababu za kuongezeka kwa shehena hizo kuwa ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa reli ya kusafirisha shehena ya mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Uganda.

Nyingine ni kufunguka kwa usafirishaji kupitia njia ya kati hususani kwa shehena inayopelekwa Uganda.

Alitaja nyingine ni kutokana na jitihada mbalimbali zilizofanyika kurejesha wateja ambao walikuwa wakisafirisha kwa kiasi kikubwa mzigo wao kwa njia ya barabara pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa sukari ya Kagera na hivyo kuongeza shehena ya bidhaa hiyo kupitia bandari ya Bukoba.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, katika kipindi hicho wamekusanya Sh. milioni 802.52.

Alitaja baadhi ya sababu za kuongezeka kwa mapato kuwa ni pamoja na kufunguka kwa njia ya Mwanza hadi Uganda, matumizi ya mfumo wa Tehama katika makusanyo, kurejea kwa shughuli za usafirishaji wa mizigo katika bandari ya Musoma.

# Bugando kujenga jengo la macho, saratani

Na Anthony Gervas, MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Bugando, jijini Mwanza, inatarajia kujenga taasisi ya magonjwa ya macho kanda na ujenzi wa wodi ya magonjwa ya saratani.

Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Prof. Abel Makubi, alisema hayo juzi katika mkutano wa watumishi na wafanyakazi wa taasisi hiyo uliojadili pia uboreshaji zaidi wa huduma za afya.

"Hospitali yetu tunatarajia kuanzisha taasisi ya macho kanda, itakaogharimu zaidi ya Sh. Bilioni 3 na ujenzi wa wodi ya saratani utakaogharimu Sh. Bilioni 1.7 zilizotolewa na serikali pamoja na wafadhili," alisema.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, wagonjwa wanaopokelewa kwa siku wameongezeka kutoka 600 mwaka 2017 hadi 1,500 mwaka 2019, huku mapato ya ndani ya hospitali yakiongezeka kutoka Sh. bilioni 1.1 hadi bilioni nne kwa mwezi.

Aidha, alisema mapato yatokanayo na dawa pekee katika hospitali hiyo yamepanda kwa mwezi kutoka Sh. milioni 400 Desemba, 2018 hadi kufikia Sh. bilioni 1.4 mwaka huu, pamoja na bima ya afya kuongezeka wagonjwa wake kutoka 100 hadi 240 kwa siku.

Prof. Makubi alisema ndoto ya ujenzi wa wodi ya saratani imekuwapo tangu mwaka 2010 ambayo sasa imetimia na kwamba huduma hospitalini hapo zitazidi kuimarika.

Kuhusu wizi wa dawa, alisema umepungua kwa asilimia kubwa baada ya kuwekwa mfumo maalumu wa kisasa wa kudhibiti tofauti na awali baadhi ya watumishi walikamatwa getini wakiwa wameficha dawa sehemu za siri na wengine kuzikalia kwenye magari wakiwa wanatoka kazini.

Mkurugenzi huyo aliwataka madaktari, wauguzi na wafanyakazi wengine kufanya kazi kwa bidii, kuwa na nidhamu kazini wakati wakitoa huduma za wagonjwa, kutoa majibu mapema ya mgonjwa bila kuchelewesha ili ajue anachoumwa baada ya kumpima.

# Ripoti yaibua madudu uchaguzi mitaa

**Na Mary Geofrey**

ASASI ya Kiraia iliyoshiriki katika uangalizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu (Tafeyoco), imewasilisha ripoti yake katika ofisi za Baraza la Vyama vya Siasa nchini, inayoelezea kuwapo kwa changamoto katika fomu za wagombea.

Ripoti inaeleza kuwa, fomu za kushiriki uchaguzi huo, zilitengenezwa na kimkakati hivyo kuwafanya wagombea wengi kushindwa kuzijaza.

Mwenyekiti Mtendaji wa Asasi hiyo inayojihusisha na wanawake na vijana, Elvice Makumbo, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, kabla ya kukabidhi ripoti hiyo kwa Mwenyekiti wa Baraza hilo, John Shibuda, alisema utafiti huo walifanya katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Alisema Dar es Salaam walifanya katika mitaa ya Buguruni na Mwananyamala na Pwani katika wilaya za Kibiti, Rufiji na Mkuranga.

Makumbo alisema katika utafiti huo, walibaini kuwa fomu za uchaguzi zilikuwa kwenye muundo wa kisheria zaidi hali iliyowafanya asilimia 80 ya wagombea kushindwa kuzijaza kikamilifu kutokana na kukosa msaada kwenye vyama vyao.

"Inawezekana fomu hizo zilitengenezwa kimkakati hivyo kufanya wengi washindwe kujaza na kama lilikuwa ni lengo lao basi lilifanikiwa," alisema Makumbo.

Alisema katika hilo walibaini kuwa hakukuwa na uhusiano mzuri kati ya viongozi wa juu wa siasa na wagombea wao hali iliyosababisha wengi wao kushindwa kuzimiza matakwa ya fomu.

Kashalika alisema asasi hiyo ilibaini kuwa vyama vya upinzani havikuwezesha wagombea wao fedha za kushiriki uchaguzi huo lakini vilishiriki kutoa maamuzi ya kutoshiriki uchaguzi.

"Hakuna uhusiano kati ya wagombea wa chini na uongozi wa juu wa vyama siasa, wagombea waliingia gharama za kushiriki uchaguzi na dosari zilipotokea viongozi wa juu wa vyama hawakuwashirikisha wagombea hili limezua manung'uniko ambayo madhara yake ni makubwa," alisema Makumbo.

Alisema madhara ya kutokuwa na ushirikiano katika maamuzi kulisababisha baadhi ya wagombea kuendelea na uchaguzi licha ya vyama vyao kususia na wagombea kuchukua maamuzi ya kuhama vyama.

Pia alisema ripoti hiyo imeeleza kwa kina kila kitu kilichotokea katika uchaguzi huo na kwamba zitawasilishwa kwa vyama19 vilivyokuwa vinashiriki uchaguzi huo kwa manufaa ya uchaguzi wa baadaye.

Kwa upande wake, Shibuda aliishukuru asasi hiyo kwa kazi kubwa waliyofanya na kusema ni wazi kuwa fomu hizo zilikuwa na 'mtego'. Alisema kutokana na Watanzania kukosa desturi ya kupambanua na kuongozwa na hisia kulifanya uchaguzi huo kuingiwa na dosari.

Shibuda ambaye ni pia Mwenyekiti wa chama cha siasa cha Ada Tadea, alisema ni ukweli usiyopingika kuwa uchaguzi huo ulikuwa na kasoro za uborongwaji na uparanganishwaji wa ndio au hapana wa kanuni.

"Kwa kuwa msema ukweli ni mpenzi wa Mungu, sasa tukiri kwamba ndani ya jamii yetu kuna gumzo la kimya kimya kuhusu fikra za kutangatanga za hoja ya kutaka kujua, kama kuna uongo au ukweli unaogusa changamoto za uchaguzi wa Serikali za Mitaa," alisema Shibuda.

Aliahidi kuwasilisha ripoti hizo kwa vyama vyote 19 vya siasa ili waisome kwa ajili ya kufanya marekebisho ya makosa kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi ujao.

Aidha, alizitaka asasi zingine kuiga mfano huo na watakuwa tayari kuendelea kupokea ripoti za aina hiyo kwa ustawi wa vyama vya siasa na demokrasia nchini.

## Watoto 64 familia duni wafanyiwa upasuaji

INATOKA UK. 3

sasa,"alibainisha.

Kwa mujibu wa Balozi huyo, wanatoa misaada kwenye sekta mbalimbali nchini ikiwamo afya, ujenzi wa vyanzo vya maji na utoaji wa elimu bure kwa wanafunzi wa Kitanzania nchini humo.

Aidha, alisema timu ya madaktari wa nchi hiyo walikuwepo nchini, walipata ushirikiano mzuri jambo liliwatia nguvu ya kufanya upasuaji kwa watu wengi zaidi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alieleza juu ya mipango yake kwa kushirikiana na taasisi hiyo kupeleka timu ya madaktari kwa ajili ya kuweka kambi mkoani Mwanza kusaidia Watanzania wengi wa eneo hilo.

Aidha, aliwataka wazazi, walezi na wadau wa sekta ya afya kujitokeza kuchangia gharama za upasuaji kwa kuwa serikali pekee haiwezi.

Kwa mujibu wa Makonda, gharama za kufanya upasuaji kwa wiki kuwa ni Sh. milioni 465 na kwamba serikali pekee haiwezi kupata fedha hizo.



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakiwa kwenye foleni ya kujiandikisha kwa ajili ya kupata vyeti vya kuzaliwa kwa maofisa wa vitambulisho Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), katika kambi maalum inayoendelea kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Laini milioni 29 bado kusajiliwa

INATOKA UK. 2

kwenye namba hii' ambalo wahalifu wa mitandao walikuwa wakiwaibia wateja fedha zao.

"Kusajili laini kwa alama za vidole imesaidia kupunguza wizi huu tunaamini kila mtu akisajili wale wahalifu wa mtaani waliohamishia uhalifu wao mtandaoni utakoma,"alisema.

"Pia kwa sababu Tanzania inakwenda kwenye uchumi wa kidigitali ni fursa kwa kila Mtanzania mwenye laini azisajili ili kuzilinda.

"Takwimu zetu zinaonyesha kwa wastani mtu mmoja anamiliki laini mbili za simu, unaruhusiwa kuwa na laini zaidi ya moja za kampuni za simu lakini uwe na sababu ya kuzimiliki na lazima mhusika ahakikishe amezisajili, kinyume chake zitakatiwa mawasiliano," alisema.

Alisisitiza kuwa hakuna mtu ambaye atakatiwa mawasiliano kwa sababu ya kuwa na laini nyingi za kampuni za simu tofauti endapo atakuwa amezisajili.

"Laini milioni 18.9 tumezisajili na namba za utambulisho milioni saba zilizotumika wengi ni wenye laini mbili au tatu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Dk. Arnord Kihaule, alisema mpaka sasa waliosajiliwa na mamlaka hiyo ni watu milioni 21.5 na ambao hawajasajiliwa ni milioni 8.3 huku namba zilizotolewa za vitambulisho zikiwa ni milioni 16.

Alisema wametoa namba za vitambulisho katika Kata 4025 za Tanzania Bara na Visiwani.

"Naomba niwatoe hofu wale ambao alama za vidole zimefutika kutokana na changamoto mbalimbali au wasio na mikono upo utaratibu uliowekwa wa usajili, hivyo watasajiliwa ili kupata kitambulisho cha taifa," alisema.

Mkurugenzi wa Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT) Sosthenes Kewe, alisema Watanzania wanatakiwa kufahamu kuwa usajili huo ni muhimu kwa sababu utamwezesha kupata kitambulisho cha taifa ambacho kitamwezesha kupata huduma nyingine bila usumbufu.

Naye Mwakilishi wa Umoja wa Mtandao wa Kampuni za Simu Tanzania (Tamnoa), Jacquiline Materu, alisema wameamua kushirikiana kuhakikisha usajili huo unakamilika kwa kila mwenye laini awe ameisajili kwa sababu halitumii hata dakika tano.

**Imeandikwa na: Romana Mallya na Maulid Mmbaga (DSJ)**



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (wa pili kulia), akikagua kabrasha za mradi wa maji wa Arusha wa Bilioni 520/- ambao vyanzo vya maji vinatoka Arumeru wakati alipowatembelea makandarasi wanaotekeleza mradi huo wilayani humo, jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wanafunzi vyuoni watakiwa kuwa wazalendo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mary Maganga, amewataka wanafunzi wa vyuo nchini, kuwa wazalendo kutokubali kutumika na watu wanaotaka kuvuruga amani ya nchi.

Aliyasema hayo jana wakati wa mahafali ya 21 ya Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), na kuwatunuku vyeti wahitimu 1,323.

Alisema wapo watu wasioitakia mema Tanzania, pia wamekuwa wakiwatumia wanafunzi wa vyuo kama sehemu ya kufanikisha malengo yao.

"Wiki ijayao tunasherehekea miaka 58, ya Uhuru na miaka 57, ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kaulimbiu ni uzalendo, uwajibikaji na ubunifu ni msingi wa ujenzi wa uchumi wa taifa," alisema Mary.

Alitoa rai kwa wanafunzi wa vyuo waliohitimu mafunzo na waliobaki vyuoni kuzingatia kaulimbiu hiyo, ili kulinda amani na mshikamano wa nchi.

Aliwataka wahitimu hao, kutumia elimu waliyoipata vyuoni kuleta matokeo chanya ya kiuchumi katika jamii kwa maslahi ya taifa.

Vile vile, aliwataka wanafunzi wa vyuo nchini kuwa na upendo, hekima, busara na waadilifu kwa watu waliowazunguka ili kuendelea kujenga misingi bora ya utamaduni wa kiafrika.

Mkuu wa Chuo hicho, Pro. Eliamani Sedoyeka, alisema chuo hicho, kinatarajia kuanzisha kozi saba mpya ya shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu, ikiwa ni mojawapo ya mikakati ya kukidhi matakwa ya Watanzania.

Pia, alisema katika kuunga mkono jitihada za serikali kwa kutekeleza ilani ya chama tawala, chuo hicho kimejipanga kutoa elimu bora kwa kuweka mazingira rafiki ya wanafunzi kusomea.

Alisema chuo hicho, kimejenga zahanati ya chuo, bwalo la chakula, jengo kwa ajili ya idara ya uzamili litakalojumuisha madarasa na kumbi za mikutano, ujenzi wa mabweni.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2019, chuo hicho kina ongezeko la wanafunzi 5,485 kutoka 3,600.

"Sisi wahadhiri na walezi tunatarajia mtatumia maarifa, ujuzi na elimu mliyoipata hapa chuoni kuwatumikia Watanzania wote kwa kuzingatia maelekezo ya Rais John Magufuli," alisema Sedoyeka.

# Wizara kutoa zabuni kwa wazawa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, amesema serikali ipo katika mpango mkakati wa kuweka sheria ya kutoa zabuni za chini ya Sh. bilioni 15, kwa makandarasi wazawa wa ili kupunguza tatizo la kukosa tenda za ujenzi wa miradi.

Kauli hiyo, aliitoa jana, mkoani hapa wakati akizungumza katika kongamano la 30, la Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET).

Alisema, utaratibu wa kuwapa zabuni makandarasi wazawa utasaidia kuondoa yao, badala yake wakipewa makandarasi kutoka nje ya nchi.

Alisema makandarasi wazawa wana uwezo mkubwa wa kutekeleza miradi mbalimbali, lakini tatizo linalowakabili ni kukosa mitaji kwa ajili ya kuifanikisha miradi.

Vile vile kuanzishwa kwa utarabu mpya wa kutoa tenda za ujenzi kwa wazawa utawasaidia kutekeleza kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Aliwataka wahandisi hao, wajifunze taaluma ya fedha ambayo itawasaidia kuendesha miradi wanayojenga.

Pia kujiendeleza zaidi na kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, pamoja na kujifunza mbinu mpya za kazi ambazo zitawafanya kuwa wabunifu.

Rais wa Chama cha Wahandisi Tanzania, Wakili Menye Manga, alisema mkutano huo, umelenga kuangalia jinsi ya kuwajengea uwezo endelevu wahandisi na kuangalia matatizo mbalimbali yanayowakabili na kutafuta ufumbuzi.

Alisema tatizo kubwa linalowakabili wahandisi hao, ni kukosa sehemu maalumu ya kufanyia mazoezi wanapohitimu kozi zao.

Wameiomba serikali kuwapatiwa eneo maalumu la kufanyia mazoezi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Manga aliwataka wahandisi hao, kusomea taaluma ya sheria kwa kuwa itawasaidia kutatua matatizo ya kisheria.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliwataka wahandisi hao kufanyakazi kwa weledi huku wakitanguliza mbele maslahi ya nchi katika hatua ya kuleta maendeleo endelevu.

# Wanahabari waaswa kuhimiza uhifadhi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAANDISHI wa habari nchini, wameombwa kutumia kalamu zao kuelimisha wananchi umuhimu wa kuhifadhi maeneo ya hifadhi na kupiga vita ujangili, ili vizazi vijavyo vinufaike na rasilimali zilizopo.

Akizungumza jana katika kongamano la tatu la Utalii lililoandaliwa na Taasisi ya Wanahabari Arusha (Arusha Media),Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Taasisi ya Chemchem, Walter Pallangyo, alisema ni vyema wanahabari wakajikita kuelimisha masuala ya uhifadhi kwa maendeleo ya taifa.

"Bila kupambana na kuhifadhi maeneo ya hifadhi yanayotuzunguka hatutafaidi rasilimali hizi na ili ziendelee kutuletea kipato na ajira lazima wanahabari mkatumia kalamu zenu kuelimisha umuhimu wa hifadhi hizi,"alisema.

Alisema taasisi yao tangu iwekeze mwaka 2018, kwenye eneo la Hifadhi ya Burunge wilayani Babati, imetumia zaidi ya Sh. milioni 165 katika vita dhidi ya ujangili.

"Majangili ni tatizo kwa kuwa katika kipindi hicho tumekamata 10 wanaojihusisha na mauaji ya tembo na majangili zaidi ya 15 wanaojihusisha na mauaji ya wanyama wengine, lengo letu kuendeleza uhifadhi," alisema.

Aliomba pia wanahabari washiriki kuelimisha madereva wanaopita barabara ya Arusha hadi Babati kuwa waangalifu, kwa kuwa baadhi yao wanagonga wanyamapori, ambao wanavuka barabara hiyo kwenda hifadhi ya Tarangile.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wanahabari ya Arusha (Arusha Media), Mussa Juma, ambaye ni muandaaji wa kongamano hilo, alisema kuna umuhimu mkubwa wa wanahabari kushirikiana na wadau wa utalii kupiga vita ujangili na vitendo vyote vinavyorudisha nyuma sekta hiyo kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Alisema kongamano hilo limedhaminiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Taasisi ya Chemchem Association na Mfuko wa Uhifadhi wa Friedkin.

# Viongozi washikiliwa upotevu wa milioni 60/-

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MKUU wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Onesmo Buswelu, ameamuru kukamatwa na kuwekwa mahabusu viongozi wanne wa chama cha ushirika cha msingi (AMCOS) cha Manio, wanaotuhumiwa kuhujumu Sh. milioni 60.8

Wanaoshikiliwa wakisubiri kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mwenyekiti, Remi Mbando na Elisante Kihundwa ambaye ni Katibu.

Wengine ni wajumbe wa bodi ya chama hicho, Barakaeli Kihundwa na Dina Kileo.

Licha ya kukamatwa kwa vigogo hao wa ushirika, pia mkuu huyo wa wilaya ameagiza kuvunjwa kwa bodi hiyo mara moja.

Uamuzi huo wa Buswelu, umekuja baada ya taarifa ya Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Siha, Heri Minja, kutoa siri hiyo mbele ya wanachama wa chama hicho kuwa kiasi cha Sh. milioni 60.8 hakionekani na wala matumizi yake hayajulikani.

Baada ya taarifa hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Siha aliamuru watu hao kukamatwa na kuwekwa ndani hadi fedha hizo zitakapopatikana

Akizungumza na wanachama wa chama hicho katika mkutano wa dharura uliofanyika katika ofisi ya chama hicho kilichopo katika Kijiji cha Manio jana, Mkuu wa Wilaya aliamuru watu hao kuwekwa ndani hadi fedha hizo zipatikane kwa kuwa wao ndiyo watendaji na wadhamini wa mali za chama.

Buswelu alisema serikali haiwezi kuona wananchi wanyonge wanauza kahawa zao ili waweze kuendesha maisha yao na familia zao wanatokea wajanja na kuwadhulumu na kwamba hawezi kufumbia macho jambo hili, huku vyombo husika vya uchunguzi vikiendeleo na kazi yao.

"Fedha hizo ziwekwe mezani kwanza, ndiyo majadiliano yaanze na ikibainika hawajahujumu, hizo fedha zitarudishwa',' alisema Buswelu. Awali, ofisa huyo katika taarifa yake alisema wanachama wa chama hicho walipeleka malalamiko kwa mkuu wa wilaya wakidaia kutolipwa mabaki ya malipo ya mwisho fedha ya mwaka 2018 na 2019 bila sababu za msingi.

Alisema wakiwa kwenye uchunguzi ili kubaini ni kiasi gani cha fedha walichotakiwa kulipwa wanachama hao ndipo walibaini na mambo mengi ikiwamo fedha hizo Sh. 60.8.

Bodi haifanyi mahesabu haifanyi mikutano kwa mujibu wa katiba kufanya ya kila baada ya miezi mitatu lakini hawafanyi .

Alisema Ihundwa ambaye ni katibu wa chama hicho, alikanusha madai hayo akidai kwamba fedha wanazodaiwa ni Sh. milioni 16 na si milioni 60.8 zinazodaiwa.

Mmoja wa wanachama hao Elisarie Elirehema alimshukuru mkuu huyo wa wilaya lakini akaeleza kuwa kuna kahawa magunia 40 yapo kwenye gharama ambayo haijaingizwa kwenye hesabu nazo ziingizwe kwenye.



Spika wa zamani wa Bunge la Tanzania, Pius Msekwa (katikati), akiwatunuku wanataaluma tisa wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Shahada ya Umahiri ya Ushirika na Maendeleo ya Jamii (MA-CCD), (hawapo pichani), katika mahafali yaliyofanyika chuoni hapo, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: GODFREY MUSH**

# Msafara wa JWTZ wakabidhiwa bendera

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKUU wa Mkoa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amemkabidhi bendera ya taifa Kanali Machera Machera, anayeongoza msafara wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), unaopeleka ujumbe maalum wa maadhimisho ya miaka 58 ya Uhuru katika kilele cha Mlima Kilimanjaro.

Maadhimisho ya sherehe za uhuru hufanyika kila mwaka Desemba 9.

Akikabidhi bendera hiyo jana katika lango la Marangu kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, Mkuu wa Mkoa, Dk.Mghwira alisema serikali inalishukuru Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa utaratibu waliojiwekea wa kila mwaka kupanda mlima huo mrefu kuliko yote Afrika kuadhimisha sherehe hizo.

Alisema uamuzi huo wa JWTZ, unaonyesha ni jinsi gani wanabeba jukumu kubwa na dhamana ya kipekee kwa niaba ya Watanzania.

Mbali na askari hao, katika msafara huo wamo pia waandishi wa habari na wafanyakazi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa).

Alisema tukio hilo linawakumbusha kile kilichofanywa na Kapteni Nyirenda mwaka 1961 ambaye alipanda kweye kilele cha Mlima Kilimanjaro na kwenda kuuweka Mwenge wa Uhuru na bendera ya taifa juu ya mlima huo maarufu duniani.

Alisema serikali inawashukuru JWTZ na watu wote waliokubali na kujitolea kupanda Mlima Kilimanjaro na kwamba inatambua mchango wa jeshi hilo ambao ni mhimili mkuu wa usalama na ulinzi wa nchi na kupanda mlima huko ni kuendeleza kujenga imani kubwa na jeshi kwa kushiriki katika matukio mbalimbali muhimu ya kitaifa.

"Muda si mrefu nitawakabidhi bendera ya taifa hivyo niwaombe mkatimize dhamira yenu ya dhati ya kufikisha bendera hiyo kileleni kazi ambayo mnaifanya kwa niaba ya umma wote wa Watanzania,"alisema Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro aliyeambatana na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM, Dk. Edmundi Mndolwa.

Alisema pia serikali inavipongeza vyombo vya habari kwa kuhakikisha wanawahabarisha wananchi taarifa mbalimbali na hivyo wanajukumu la kuwakumbusha Watanzania juu ya umuhimu wa historia ya uhuru kupitia kupanda mlima huo na kutoa habari zinazohamasisha uhifadhi wa mali asili na kutoa taarifa za kutangaza utalii.

Mghwira alisema Tanapa ni moja kati ya mashirika ya mfano wa kuigwa nchini kwa utendaji kazi mzuri na sasa Watanzania wameshuhudia wakiongeza hifadhi sita zaidi za kusimamia hivyo kufanya jumla ya hifadhi za taifa kuwa 22.

Kamishina Mwandamizi wa Uhifadhi Kanda ya Kaskazini Herman Batiho, alisema Tanapa itaendelea kuadhimisha maadhimisho ya siku ya uhuru kuenzi kazi zilizofanywa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kuleta uhuru wa taifa.

## Kaya zote Rombo sasa zina umeme

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

SHIRIKA la umeme Tanesco limeeleza kuwa kila kaya ya Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, imeunganishwa na umeme.

Meneja wa Tanesco Wilaya ya Rombo, Mhandisi Hassan Lumuli, alisema nia ya serikali ya kufikisha umeme katika kila kijiji imeshatimia katika wilaya hiyo.

Alikuwa akitoa taarifa katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Wilaya kilichofanyika jana.

Katika taarifa yake, Mhandisi Lumuli alisema mpaka sasa kwa asilimia mia moja, kata zote na vijiji vyote vya Rombo vimeshafikiwa na umeme.

Aidha, alieleza kuwa kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Oktoba 31, mwaka huu jumla ya wateja 2,842 wameunganishiwa na huduma hiyo.

Kwa mujibu wa Mhandisi Lumuli, hadi kufikia Oktoba 31 mwaka huu, wananchi 25,346 walikuwa wameshaunganishiwa umeme.

Pamoja na hilo alilieleza baraza hilo kuwa wananchi ambao bado hawajaunganishiwa umeme, wanaweza kuunganishwa na huduma hiyo kwa bei elekezi ya serikali ya Sh. 27,000 kwa maeneo ya vijijini.

Katika hatua nyingine, Mhandisi Lumuli litoa rai kwa wananchi kutokuwa na hofu ya kufungua viwanda kwa sababu Tanesco Rombo bado ina uwezo wa kuwahudumia.

Lumuli alisisitiza kuwa wilaya hiyo inacho bado kiasi cha megawati 1.5 za umeme ambao hauna matumizi hivyo watu wachangamke kuutumia.

Wakati matumizi makubwa ya umeme katika Wilaya ya Rombo ni megawati 3.0, lakini kiasi kinachofikishwa ni megawati 4.5.





Ofisa Mwandamizi wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Philiphina Kobelo (kushoto), akitoa mafunzo ya elimu ya maadili kwa viongozi wa serikali za kata, vijiji na vitongoji (hawapo pichani), katika Kata ya Mvumi Misheni wilayani Chamwino, Mkoa wa Dodoma jana. Kulia ni Ofisa wa maadili sekretarieti hiyo, Grece Kwambiana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waomba mafunzo Tume ya Maadili

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

VIONGOZI wa serikali za vijiji na vitongoji wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wameiomba Tume ya maadili ya viongozi wa umma kuwapatia mafunzo ya elimu elekezi ya maadili ya viongozi wa umma ili wafanye kazi kwa kufuata miongozo ya jinsi ya kuwatumikia wananchi.

Maombi hayo yalitolewa kwa nyakati tofauti na viongozi wa kata za Mlowa Barabarani na Mvumi Misheni, mbele ya watumishi wa Tume hiyo, baada ya kupatiwa elimu ya mafunzo ya maadili yaliyotolewa kwa ajili ya viongozi wa serikali za vijiji na vitongoji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti viongozi hao wa serikali za vijiji na vitongoji, walisema ili waongoze wananchi kwa kufuata miongozo ya kimaadili wameomba kupewa mafunzo hayo ambayo yatawawezesha kuwatumikia kwa kufuata kanuni, sheria na muongozo wa katiba ya nchi.

George Mahembe, Mwenyekiti wa serikali ya kijiji cha Chihembe, kata ya Mvumi Misheni, alisema elimu hiyo ikitolewa itawasaidia kukabiliana na namna ya kuepukana na migogoro inayokwamisha maendeleo ya wananchi.

"Sisi kama mabalozi wa serikali tunaoongoza vijiji na vitongoji tukielimishwa kwa kupitia Tume hii ya maadili ya viongozi ni imani yetu tutawatumikia wananchi kwa kufuata kanuni na miongozo kwa uwazi na wao watafahamu hata pale tunapokosea wapi pa kupeleka malalamiko yao," alisema.

Ruth Jeremia, kutoka kata ya Mlowa Barabara, alisema viongozi wa serikali za mitaa wanatakiwa kupewa mafunzo hayo kabla ya kuanza kuwatumikia wananchi kwa kuwa wengi wao wakishapewa nafasi hizo za uongozi huanza kuwadharau na ubaguzi hata katika itikadi za kisiasa.

Hata hivyo, alisema baadhi ya viongozi hawafuatilii malalamiko ya wananchi yanapotolewa kwenye vikao vya kijiji na vitongoji hasa yanayohusu migogoro ya ardhi inapojitokeza.

Alisema mafunzo hayo yatawawezesha kutambua wajibu wao jinsi ya kutatua migogoro hiyo, ikizingatiwa kuwa tayari watakuwa wameshapatiwa mafunzo hayo.

Kwa upande wake Ofisa wa sekretarieti ya viongozi wa umma kutoka ofisi ya Rais, Grace Kwambiana, aliwataka viongozi kuwatumikia wananchi bila upendeleo ili kuaminiwa zaidi, badala ya kutumia nafasi hiyo kwa maslahi yao binafsi.

Akizungumza na viongozi wa serikali Kata ya Mvumi Misheni, aliwataka kutumia nafasi walizochaguliwa kwa malengo ya kuisadia serikali katika kuleta maendeleo ili watu wake wafikie hatua ya uchumi ambao utawawezesha kulinda amani ya nchi.

# Takukuru yatakiwa kupambana rushwa uchaguzi 2020

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, ameagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) kupanga mikakati kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa 2020, ambako alisema kuna vitendo vingi vya rushwa vya kuwarubuni wananchi.

Pia, Takukuru imefanikiwa kurejesha Sh. milion 950 za mazao ya wakulima zilizoibiwa na vyama mbalimbali vya ushirika nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Takukuru wenye kaulimbiu ya kupambana na rushwa ni wajibu wa kila mmoja, waziri Mkuchika alisema pamoja na kuwa wamefanikiwa asilimia 88.1 katika uchaguzi uliopita wa serikali za mitaa, ichukuliwe kama kipima joto kwa ajili ya kujiandaa na uchaguzi mkuu ujao ambao kuna rushwa nyingi.

Mkuchika alisema uchaguzi huo ni muhimu kwa sababu ndiyo unachagua viongozi wa ngazi ya juu akiwamo rais, wabunge na viongozi wengine hivyo kuchagua wala rushwa itakuwa vigumu kuliongoza taifa hususani kwenye usimamiaji wa vyakula.

Alisema ipo haja kubwa ya kujipanga vyema katika kufuatilia vitendo vya uchaguzi huo rushwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2020.

Alisema uchaguzi huo unapaswa kuendeshwa na kusimamiwa kwa uadilifu na umakini mkubwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili haki, usawa uhuru na demokrasia viweze kustawi kuendelezwa na kudumishwa.

"Rushwa katika uchaguzi ni zaidi ya udanganyifu wa hesabu za kura, ambayo ikitendeka inasababisha kukosa viongozi waadilifu, wazalendo na wenye uvunjifu wa amani kutokana na migogoro ya mara kwa mara ya kisiasa," alisema Mkuchika.

"Viongozi kukosa uwajibikaji, kufanya uamuzi ya kisera yenye maslahi ya wachache, kukosekana kwa uwazi wa maamuzi ikiwamo utawala bora na wananchi kukosa imani huchangia na rushwa," alisema Mkuchika.

Alifafanua zaidi kuwa tayari wameanza maandalizi katika eneo hilo ndiyo maana Aprili, mwaka huu walifanya warsha iliyokusanya wadau kutoka katika kila sekta ili wapange mikakati ya kudhibiti vitendo vya rushwa.

Vile vile, aliwataka Takukuru kuweka mkazo katika suala la rushwa ya ngono ambalo limekuwa kero na kuibuliwa kwenye vyombo vya habari.

"Nawaomba Takukuru simamieni rushwa ya ngono vyuoni na kwingineko, hivi karibuni Makamu Mkuu wa Chuo kikuu UDOM alikiri rushwa ipo vyuoni, hivyo fuatilieni na kuwataka wanafunzi wa kike nao kutoa taarifa pale wanapokutana na rushwa hizo,"alisema Mkuchika.

Alisema imefahamika watuhumiwa ambao wanalawiti watoto wakikamatwa, wazazi wanakaa meza moja kujadili suala hilo na kulimaliza bila hatua yoyote kuchukuliwa jambo ambalo halikubaliki.

"Ikibainika mzazi anafanya kitendo hicho yeye na mtuhumiwa wote watachukuliwa hatua kali," alisema Mkuchika.

Alisema wanawake wapo wengi iweje mwanaume aende kubaka watoto au kulawiti na kuwasababisha magonjwa ya kuambukiza vijana wadogo ambao ni taifa la kesho.

Kwa upande wa vyama vya ushirika, Mkuchika aliwataka Takukuru kuvifuatilia vyama hivyo ambavyo vimekuwa kichaka cha wezi na wala rushwa na kutowatendea haki wakulima.

Alisema amefurahi kuona Takukuru wameshirikiana na wadau kupambana na rushwa, ikiwamo kuzindua kampeni ya Utatu iliyofanyika Novemba Mosi, hivyo anaamini jitihada hizo zitaendelea katika kuvunja ukimya wa kukataa rushwa.

# Serikali yabaini madudu ununuzi wa umma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kwa mwaka 2018/19 inaonyesha mikataba 12, kutoka taasisi tisa za umma yenye thamani ya Sh. bilioni 25.8 ina viashiria vya rushwa kwa sababu haikufuata taratibu.

Akizungumza katika mkutano wa 10, wa wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Naibu waziri wa fedha Dk. Ashatu Kijaji, alisema kuwa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa ununuzi wa jumla ya Sh. bilioni 16.6 haukuwa kwenye bajeti wala mpango wa ununuzi ulioidhinishwa na Sh. bilioni 24.85 zimetumika kulipa mikataba ambayo haikuwa na hati ya utekelezaji.

Dk. Kijaji aliwataka waajiri wote kutoa ushirikiano kwa bodi za kitaaluma hususan linapojitokeza suala la usimamizi wa maadili kwa wataalamu waliosajiliwa na bodi husika, kwa kuwa hakuna ufanisi bila maadili. Ameupongeza uongozi wa Bodi ya ugavi na manunuzi (PSPTB) kwa hatua zilizochukuliwa za kusimamia mahitaji ya ajira ya kada ya ununuzi na ugavi kwa kuwapeleka mahakamani watu wanaofanya kazi za ununuzi na ugavi bila kuwa na sifa stahiki.

Aliagiza waajiri wote kuwaajiri watumishi wenye sifa zinazotambuliwa na PSPTB na kuzingatia mahitaji yaliyopo kwenye waraka wa maendeleo ya utumishi wa mwaka 2015.

Naibu waziri huyo, ameiagiza Bodi ya PSPTB kufanya tathmini ya uwezo na uadilifu wa taasisi za umma zilizobeba dhamana ya ununuzi serikalini.

Alielekeza kuwa taarifa ya Baraza la Maadili iwasilishwe wizarani mapema ili iweze kupitiwa na kufanya uamuzi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya serikali.

Alisema pia Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kuunga mkono juhudi za Bodi zinazolenga kuondoa uzembe na ukiukwaji wa maadili katika fani ya ununuzi na ugavi, kwa kuwa bajeti ya ununuzi wa serikali ni takribani asilimia 80 ya bajeti yote.

Kwa upande wake Kamishna wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma, Dk. Fredrick Mwakimbinga, alisema kuwa Bodi inafanya jitihada za dhati kuhakikisha taaluma ya ununuzi na ugavi inatoa mchango unaotarajiwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kulingana na malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano, ili kutimiza malengo hayo bodi imetoa mafunzo mahususi kwa taasisi mbalimbali ambayo yameongeza ufanisi katika taasisi husika.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB, Godfrey Mbanyi, alisema kuwa Bodi hiyo imeahidi kufanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na Naibu Waziri Dk. Kijaji.

Alibainisha kuwa licha ya kuwa na sheria inayowataka watumishi wanaofanya kazi ya ununuzi na ugavi kusajiliwa, bado wapo ambao hawafanyi hivyo, Bodi itaendelea kuchukua hatua stahiki kwa wale wote watakao kiuka sheria.

Dk. Kijaji akielezea kuhusiana na agizo alilotoa katika mkutano wa 10 wa wataalamu wa ununuzi na ugavi kutoka maeneo mbalimbali alisema kuwa, kuna ununuzi usiozingatia sheria na kanuni na kusababisha kununua bidhaa zilizo chini ya kiwango, ununuzi hewa wa huduma na bidhaa na kutokuwepo kwa kumbukumbu za ununuzi na mikataba hewa licha ya uwepo wa wataalam hao.



## HABARI ZANZIBAR



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akizungumza na wanafunzi wa shule ya sekondari Chumbuni, wakati alipofika shuleni hapo kwa ajili ya kuangalia maendeleo ya wanafunzi hao wanaofanya mitihani yao ya kidato cha pili. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Smida kuwaendeleza wafanyabiashara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda imesema wakala wa kuendeleza viwanda vidogo na vya kati (Smida) ndiyo yenye jukumu la kuwaendeleza wafanyabiashara na wajasiriamali nchini ili kufikia malengo ya kujitegemea.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, aliyetaka kujua kazi za Smida kama zinafahamika na wananchi.

Alieleza kuwa Smida ipo kwa mujibu wa sheria na imepewa majukumu ya kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo kufikia ngazi za kuwa wajasiriamali wakubwa. Alisema taasisi hiyo imepewa majukumu ya kuwapatia ujuzi na mbinu za kitaalamu pamoja na mikopo wajasiriamali kufikia ndoto za kupiga hatua kubwa ya maendeleo. "Hayo ndiyo majukumu ya wakala wa kukuza viwanda vidogo na kati kwa wajasiriamali mbalimbali Unguja na Pemba ili malengo ya kufikia nchi ya uchumi wa kati yanafikiwa," alisema. Alisema tayari wakuu wa mikoa na wilaya wametakiwa kutenga maeneo ambayo yatatumiwa kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya wajasiriamali mbalimbali na kuzalisha bidhaa zao. "Tunataka kila wilaya kutenga maeneo ambayo yatatumiwa kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya wajasiriamali wadogo nchini," alisema.

# Serikali yapiga marufuku uvamizi misitu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, imepiga marufuku vitendo vya uvamizi wa msitu wa hifadhi wa Ngezi Pemba na baadhi ya watu hufanya uharibifu ikiwamo kukata miti kwa shughuli za mbao.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la ChakeChake, Suleiman Sarhani, aliyetaka kujua mikakati inayochukuliwa na serikali kukabiliana na uvamizi wa msitu wa Ngezi Pemba. Alikiri kuwapo matukio ya baadhi ya watu kupenya katika msitu huo na kufanya uharibifu wa msitu ikiwamo kukata miti kwa matumizi ya mbao.

Aliwataka wananchi kufahamu kuwa msitu wa Ngezi unalindwa chini ya sheria ya misitu iliopo katika hifadhi ya kitaifa na hauruhusiwi kufanyika matukio ya uharibifu na kukata miti.

"Msitu wa Ngezi upo chini ya sheria ya misitu ya hifadhi ya taifa na wananchi hawatakiwi kuingia na kukata miti katika eneo hilo," alisema.

Alisema juhudi zimeanza kuchukuliwa ikiwamo kuajiri walinzi kwa ajili ya kukabiliana na uharibifu huo ikiwamo kufanya doria katika maeneo ya Unguja na Pemba.

"Wizara ipo katika hatua za mwisho kukamilisha ajira kupata walinzi watakaofanya doria katika msitu huo na kukabiliana na matukio ya vitendo vya uharibifu wa mazingira," alisema.

# Wanafunzi waonywa udanganyifu kwenye mitihani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi wa kidato cha pili wanaoendelea na mitihani yao ya taifa, kutojihusisha na udanganyifu ili waweze kufaulu vizuri katika masomo yao.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wanafunzi wa shule mbalimbali za mjini Unguja wa kidato hicho walioanza mitihani yao juzi. "Fanyeni mitihani yenu kwa kutumia akili zenu na msifanye udanganyifu wa aina yoyote," alisema Waziri huyo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafanya kila jitihada kujenga shule za kisasa, upatikanaji wa madawati pamoja na kutoa elimu bure kuanzia ngazi ya maandalizi hadi kidato cha nne.

Alisema kuwa lengo la serikali kutoa elimu bure ni kuhakikisha kila mwananchi anapata elimu bila ya ubaguzi.

Aliwataka wanafunzi hao kuzitumia vizuri fursa hizo kwa kuzidisha bidii ya kusoma ili waweze kufanikiwa ndani ya maisha yao, pamoja na kusaidia nchi kuwa na wasomi wake.

Aliwataka wazazi na walezi kuwa karibu zaidi na watoto wao wanaofanya mitihani hiyo ili kuhakikisha wanafika katika vituo vyao vya mitihani kwa wakati na kutumia haki yao ya elimu.

"Wizara inawaomba madereva na utingo wa gari za abiria kuzidisha busara na hekima kwa wanafunzi wakati wa kwenda na kurudi shule ili kuwahi shule na kufanya mitihani yao vizuri," alisema.

Alieleza kuwa ufanyaji wa mitihani unahitaji amani na utulivu hivyo ameiasa jamii kuwa asiyehusika asijaribu kusogea kituo cha mitihani kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria na kanuni za mitihani.

Jumla ya wanafunzi 34,469 wanafanya mitihani yao wanawake wakiwa 18,502 na wanaume ni 15,967 sawa na upungufu asilimia moja ikilinganishwa na idadi ya watahiniwa waliofanya mitihani mwaka jana.



**JAPHET**

Soma UK.14

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI DESEMBA 7, 2019



# KUNANI TENA?

## SHAMSA, NAY WA MITEGO MOYO WADUNDA

Soma UK.15

## BASI SAWA



# Wolper anogewa Arusha kifedha

MWIGIZAJI wa Bongo Muvi, Jackline Wolper, amesema ameamua kuyaaga maisha ya Tandika jijini Dar es Salaam kutokana na hadhi yake kupanda.

Wolper amesema maisha yake kwa sasa yapo Arusha ambako kuna watu wenye hadhi kama yake na huko ataweza kuishi bila kuingiliwa kama alivyokuwa akiishi Dar.

"Unajua maisha ya Tandika yapo tofauti, nimeamua kwenda Arusha baada ya hadhi yangu kupanda na kule ninaishi na wezangu wenye fedha hatuwezi kufuatiliana," amesema Wolper.



# MC Mziwanda atangaza 'Mungu Yupo Hapa'

MSHEREHESHAJI maarufu jijini Mwanza, MC Mziwanda amekamilisha vídeo zá nyimbo mbili ikiwa ni maandalizi ya albamu yake ya nyimbo za injili aliyoipa jina la 'Mungu Yuko Hapa'.

MC Mziwanda amezitaja nyimbo hizo kuwa ni 'Sema Nasi' na 'Shuka Baba, ambazo amemshirikisha vídeo Queen Sonia Boniface.

" Wiki ijayo nitashuti vídeo ya wimbo wa tatu nilioupa jina la Ulinzi ikiwa ni mwendelezo wa kukamilisha albamu yangu itakayokuwa na nyimbo nane, " amesema MC Mziwanda.

Amesema ameamua kuonyesha kipaji chake upande wa kuimba ingawa wengi wamezoea kumuona akifanya kazi ya ushereheshaji.

# JAPHET FELIX

## MWANAMUZIKI WA INJILI ANAYEKUJA MOTO



MSANII chipukizi wa nyimbo za Injili, Japhet Felix (32) amesema kufanya kazi ya kumtumikia Mungu kupitia muziki ni lazima uwe na moyo mgumu na uwe tayari kukabiliana na vikwazo.

Akizungumza katika mahojiano maalum na BT, Felix amesema baadhi ya watu walioingia katika muziki huo wamejikuta wakiishia njiani kutokana na kushindwa kuhimili majaribu.

Amsema kwa upande wake amepata mafanikio tangu aanze kuimba Injili miaka mitatu ilyopita na tayari anaandaa Albam yake ya kwanza itakayotoka mapema mwakani.

**ALIANZIA WAPI?**

Felix alisema alipoanza kuimba Injili alikabiliwa na vikwazo vya kifedha na wakati mwingine alishindwa kurekodi kutokana na kukosa pesa.

Anasema anamshukuru mama yake kwa kumpa moyo jambo ambalo lilimfanya kuwa na bidii hadi alipotoa wimbo wake wa kwanza "Kinga" ambao unatamba kwa sasa.

Anasema anamshukuru Mungu mpaka sasa anaendelea kumtumikia kwa kuimba nyimbo ambazo watu wakizisikiliza kwa umakini wanaweza kubadilika.

**WANAMUZIKI ANAOWAPENDA**

Amesema katika muziki wa Injili kuna wanamuziki kadhaa ambao anawapenda na ndio muongozo wake kwa kila anachokifanya ili kuongeza mashabiki wake.

Amewataja wasanii hao kuwa ni Goodluck Gozbert, Rose Mhando, Christine Shusho na Bon Mwaitege.

**USHAURI WAKE**

Felix ametoa ushauri kwa wanamuziki wa fani hiyo kuweka mbele utu na umoja kwani muziki huo unalenga kuweka usawa bila kujali hadhi ya mtu husika.

"Tuache majungu, kutengana na kununiana kwani vitu hivi vitaturudisha nyuma na kuondoa dhana halisi kwamba muziki wa Injili ni neno la Mungu na tunahitajika kulieneza kwa upendo," amesema Felix.

## INSTA-TWITTER





**Kuna** sehemu natakiwa niwepo, naomba Mungu anifikishe huko. Mimi kama binadamu peke yangu siwezi, nakutana na vishawishi vingi dah ila najua mimi si chochote mbele ya Mwenyezi Mungu-**Shamsa Ford.**



**Tunamalizia** mapicha picha, sema Mwakinyo anapatikana wapi? Nina zawadi yake mtoto wa kitanga Yule-**Amber Lulu.**



## KUNANI TENA? Shamsa, Nay wa Mitego moyo wadunda

UTATA umetanda kati ya wasanii Nay wa Mitego na Shamsa Ford, kutokana na kuwa karibu kwa kipindi hiki kiasi ambacho inahusisha wawili hao kurudisha mapenzi.

Moja kati ya video ambayo inazungumziwa kwa sasa ni ile ya muigizaji wa filamu Shamsa Ford na msanii wa muziki Nay wa Mitego, ikiwaonesha wakiwa dukani wakifurahi na kuongea kwa pamoja.

Video hiyo aliiweka Shamsa Ford, kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram, imezidisha wasiwasi wa mashabiki wao kwamba kuna kitu kinaendelea kati yao bali hawajaamua kuweka wazi.

"Kuachana si bifu jamani mnaachana kwa amani na upendo na kila mmoja amuombee kheri mwenzie, sisi vijana na tunategemeana kwenye kazi nyingi za kujenga Taifa letu, ahsante kwa kuja binamu yangu" ameandika Shamsa Ford kusindikiza video hiyo.

Shamsa na Nay wa mitego walikuwa wapenzi kabla ya kuachana. Shamsa aliamua kufunga ndoa na Chidi Mapenzi na waliachana mwaka huu.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**



## MKE WANGU SI MSHUMAA
# KIBA AWAWAKIA WANAOMSAKAMA


MWANAMUZIKI Ali Kiba, amefafanua kwamba wimbo wa 'Mshumaa' haukumlenga mkewe ambaye sasa wametengana kwani aliutunga miaka mitatu iliyopita.

Kiba alisema mke wake alikuwa alipenda wimbo huo na mara kwa mara aliimba, hivyo aliomba watu wasikuze mambo hayo.


"Kila ndoa kuna kutofautiana, mimi na mke wangu tulitofautiana lakini tumeweka jambo hili, naomba watu wasihusishe Mshumaa na mke wangu kwani niliutunga wakati yeye yupo na anaupenda sana.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Uhusiano** kati ya maji na samaki umenifanya niamini usaliti upo. Ni baada yakuona maji yanapika samaki-**Irene Uwoya.**



**Huwezi** sema unaacha pombe, basi unataka baa zote duniani zifungwe, utachekesha umati! Ufanyapo jambo lako, fanya kimpango wako.Usitegemee kila mtu atafanya utakalo wewe. utakwama-**Ray C.**



**Bora** uwe na marafiki waliokuzidi. Chagua marafiki wenye tabia nzuri kuliko yako, wenye maendeleo kukuzidi, ndiyo utapata changamoto na kupambana kuwafikia. Lakini ukiwa na rafiki levo moja, huwezi kufanikiwa maana ni ngumu sana kipofu kumuongoza kipofu mwenzie. Mtaishia kupotea tu-**Chuchu Hans.**

# Kuumbe!



# LIL BUB

## PAKA MBURUDISHAJI ALIYEKUSANYA PESA NYINGI

LIL Bub ni jina la paka ambaye ndiye anaongoza kuwa na wafuasi zaidi ya milioni mbili katika mtandao wa Instagram.

Bub ndiye paka mwenye umaarufu mkubwa zaidi mtandaoni kutokana na umbo lake na vituko vyake ambavyo viliwaburudisha mamilioni ya wafuasi wake katika mitandao mbalimbali ya kijamii.

Hata hivyo Bub amefariki hivi karibuni na mmiliki wake Mike Bridavsky amethibitisha kupitia akaunti yake ya Instagram. Kifo chake kimewashtua wafuasi wake ambao walimpenda kwa mtindo wake wa kutoa ulimi nje.

BUB NI NANI?

Bub ni paka ambaye aliokotwa akiwa ametelekezwa huku akiwa na ulemavu wa aina mbali mbali. Lakini pia alikuwa amedumaa hivyo siku zote alionekana kama paka mtoto. SHAPE * MERGEFORMAT

Mmiliki wake anasema paka huyo amesaidia kupatikana kwa kiasi cha dola za kimarekani laki saba kipindi chote cha maisha yake kwa ajili ya kusaidia wanyama wengine.

"Bub ameleta mabadiliko makubwa sana katika ulimwengu salama wa wanyama na katika maisha ya watu ulimwenguni" moja kati ya ujumbe wa Instagram punde baada ya kutangazwa kifo chake.

Mmiliki wake bwana Bridavsky alimuasili Bub kutoka kwa rafiki yake ambaye alimuokota katika eneo lenye vifaa chakavu huko Indiana.

Mwaka 2011 alitengeneza blog kupitia Tumblr kwa ajili ya paka huyo, ghafla picha za Bub zikasambaa mtandaoni kama moto hii ni baada ya picha moja ya bub kuwekwa katika ukurasa wa mbele wa tovuti ya majadiliano ya Reddit.

"Bub alikuwa mpole na mwenye upendo sana" mmiliki wake alisema

Picha yake ilizua majadiliano makubwa sana hali iliyopelekea kuandikwa kwa taarifa zake katika magazeti ikiwepo kupewa mualiko katika kipindi kimoja cha televisheni nchini Marekani.

Bub akaanza kuingia mikataba na kampuni mbali mbali huku mmiliki wake akimuandalia kipindi chake katika You Tube ambacho kilikuwa burudani tosha kwa mashabiki wake.

Na kutumia umaarufu wa paka wake huyo, alikusanya pesa kwaajili ya kuwasaidia paka wengine wenye mahitaji maalumu. SHAPE * MERGEFORMAT



# Marapa waliotingisha dansi




**Na Adam Fungamwango**

KURAP kwenye muziki wa dansi kunatofautiana sana na kwenye muziki wa kizazi kipya. Marapa wa Bongofleva ni wale ambao wanaimba kwa kufokafoka, maarufu kama watu wa hip hop.

Tukirejea kwenye muziki wa dansi, mwanzoni mwa miaka ya 2000 nchini Tanzania kuliingia aina ya muziki ambayo baada ya waimbaji kumaliza kazi yao na kuingiza ala za muziki, katikati yake kuliwekwa vionjo ambavyo vilisababisha muziki kuchangamka zaidi.

Asili ya 'kurap' katikati ya ala za muziki ni nchini Congo DR, na ililetwa na bendi inayopendwa sana nchini humo Zaiko Langalanga. Hiyo ilisababisha bendi zingine ziige mfumo huo kutoka ule wa rhumba ambao vyombo vinasikika peke yake bila maneno.

Marapa wawili wa Zaiko Langalanga, walikuwa wakisherehesha katikati ya muziki kwa kusema 'atalaku atalaku' na ndiyo maana nchini humo marapa hadi leo wanajulikana kwa jina la Atalaku.

Hawa ni baadhi ya mapara nchini waliotamba kwenye bendi mbalimbali kwa kunogesha muziki.

**Allan Mulumba Kashama**

Huyu ni Mkongomani, lakini alikuwa mmoja wa wanamuziki wa mwanzo kabisa Tanzania kufanya kazi ya kurap kwenye bendi za muziki wa dansi.

Akiwa na bendi ya Diamond Sound wana Dar es Salaam Ikindankoi alijipatia umaarufu sana kwa staili yake ya kurapu, 'amevaa kimini amevaa bodi suti'. Nyimbo kama "Neema', 'Kimalumalu' na zingine ambazo zilikuwa maarufu mno mwishoni mwa miaka ya '90 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, zilimuweka kwenye chati ya juu na kuheshimika kwa kazi hiyo.

**Msafiri Doif**

Kwenye bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta' kulikuwa na wanamuziki ambao walikuwa wakiimba, lakini pia wakimaliza kuimba wanarap, lakini hawakuwa marapa halisi.

Hao ni Banza Stone na Ally choki ambao kiasili si marapa bali ni waimbaji. Lakini kwa mara ya kwanza, Twanga Pepeta ilimpokea rapa halisi kutoka Kenya, Msafiri Diof, Mtanzania ambaye alikwenda kutafuta maisha na kuamua kurejea nchini.

Ni rapa kwa kiwango cha juu, amejipatia sifa kubwa akiwa kwenye bendi hiyo ambayo hadi leo badi yupo.

**Totoo Ze Bingwa**

Mwenyewe anajiita rapig mia saba sabini na saba katika siku saba. Huyu ni Mkongomani anayefanya kazi nchini na amepitia bendi mbalimbali za dansi kubwa zikiwemo FM Academia, Akudo Impact na zingine.

Ametoa mchango mkubwa wa muziki wa dansi, hasa kwenye staili ya kurap. Kwa sasa ana kundi lake la Sanaa, Sana Band.

**Kalala Junior**

Ni mtoto wa mwanamuziki nguli nchini Hamza Kalala. Pamoja na kwamba Kalala Junior ni mwimbaji, lakini alianza muziki kama rapa na vile vile anakofanya vizuri zaidi na mashabiki wake wengi hupenda zaidi anavyorap. Amewahi kupitia bendi mbalimbali kama Bambino Sound, lakini kwa muda mrefu yuko na Twanga Pepeta hadi sasa.

**Khalid Chokoraa**

Kilikuwa kizazi fulani hivi cha pili cha marapa ambacho kiliibuka baada ya Ally Choki kwenda kuunda bendi ya Extra Musica. Nyimbo za bendi hiyo na aina yake ya kurap, ilitishia bendi nyingi za staili hiyo. Hadi leo amekuwa mmoja wa marapa bora kabisa nchini Tanzania.

# IMETOKEA

# Lady Gaga aporomoka jukwaani

OKTOBA 2019, mwanamuziki wa Marekani, Lady Gaga, alitawala vyombo vya habari baada ya tukio la kuporomoka jukwaani wakati wa onyesho lake la muziki.

Tukio hilo lilitokea jijini Las Vegas, wakati mashabiki wake wakiwa katika kilele cha burudani huku wakizidiwa na utamu wa nyimbo zake.

Gaga alianguka kutoka juu ya jukwaa hadi chini kwa mashabiki wake baada ya jaribio la kukumbatiana na shabiki wake kushindikana.

Awali alimuita shabiki wake kwa jina Jack kwa nia ya kujumuika naye jukwaani na kumrukia mikononi mwake.

Lakini Jack hakuwa imara na wawili hao walianguka chini kama kifusi cha udongo.

Baada ya muda Lady Gaga alirejea na kutumbuiza kibao chake kiitwacho Million Reasons akiwa sambamba na shabiki huyo.

Mashabiki walikuwa wakifuatilia hali ya Gaga kwa kuwa ana matatizo ya baridi hali inayomsababishia maumivu makali sana.

Mwaka 2013, aliahirisha onyesho lake la Born This Way baada ya kuteguka nyonga. Lakini muimbaji huyo aliwapa moyo mashabiki wakati walinzi walipomsaidia kunyanyuka.


Pia Nyota huyo alimpa moyo Jack, ambaye alikuwa akilia baada ya tukio hilo.

"Usiwe na wasiwasi, kila kitu kiko sawa. si makosa yako," alisema Gaga na kuongeza "Unaweza kuniahidi kitu? unaweza kuacha kujilaumu kwa kile kilichotokea?"

Baadae kwenye onyesho hilo, Gaga alithibitisha kuwa ajali hiyo haijasababisha madhara yoyote, alipotumbuiza kibao chake, Bad Romance.









# Tattoo

## Mapenzi hayashikiki, ila huonekana

**Na Adam Fungamwango**

PENZI ni kitu cha ajabu sana. wazee wa zamani wanasema mwenye kupenda haoni wala hasikii.

Kwenye penzi mwenye pengo huona mwanya na kwenye chongo kuna kengeza.

Penzi ndiyo kitu pekee duniani kinachoweza kumtoa binadamu anayekaa Oysterbay au Masaki na kwenda kuishi Manzese, Tandale au Kigogo bila kuona tofauti yoyote ile.

Penzi la ukweli siku zote huonekana zaidi kuliko kusikika. Ukiiangalia na kuifuatilia filamu hii ya 'Tatoo' inaoyesha na kuthibitisha imethibitisha maneno haya.

Imechezwa na wasanii Elizabeth Michael "lulu', Charles Magari, Hasnat Mathius, Mandela Nicholaus, Grace Mapunda na wengine wengi.

Inaanza kuonyesha kuwa Dastan, kijana wa kimasikini akimpenda Nicol, binti wa mzaa Magari ambaye ni tajiri.

Mzee Magari alipokuja kugundua uhusiano hiyo, hakuupenda kytokana na tofauti hizo za kitabaka.

Kuna siku akawavizia, akawabamba, akawakimbiza.Dastan anakimbia, lakini anaanguka na kuumia.

Anaporudi nyumbani, mzee Magari anampiga binti yake. Kwa hasira naye anakunywa sumu.

Habari zinamfikia Dastan, lakini hawezi kwenda msibani, badala yake baada ya mazishi anaamua kwenda kwenye kaburi la mpenzi wake.

Kwa bahati mbaya anakutwa na mzee Magari ambaye anampiga hadi kudondokea ukuta wa kaburi na kuzirai.

Madaktari wanashindwa kumtibia Dastan na kuamua kumpeleka kwenye wodi wa vichaa kwa uchunguzi zaidi.

Nyumbani kwa mzee Magari nako mambo sasa yanaanza kubadilika. Kijana wa wake Neron anamgeukia baba yake na kumwambia ukweli kuwa ana roho mbaya kwa sababu amesababisha kifo cha dada yake Nicol kwa kumtakaza kuwa na mpenzi anayempenda, hivyo akamwambia na yeye anaondoka nyumbani hapo ili akae kwenye nyumba yake ya kitajiri peke yake.

Naye anaamua kwenda kuishi na mpenzi wake ambaye ni masikini, Lulu. Huko Neron na mpenzi wake Lulu wanapanga mikakati ya kumuokoa Dastan kwenye hali yake ya kuchanganyikiwa.

Kwanza Lulu anajichora tatoo ambaye imefanana na ile aliyejichora marehemu Nicol wakati wa uhai wake. Halafu anajifanya kichaa ili apate nafasi ya kukutana na Dastan kwenye wodi yao.

Mpango huo unawahusisha pia madaktari ambao nao wanakula dili. Lulu anapachikwa hospitalini kwenye wodi ya vichaa, baada ya kujifanya kuwa amechanganyikiwa.

Baada ya kituko vya hapa na pale Lulu kumuonyesha Dastan tatoo kila wanapokutana, hatimaye kijana huyo anarejesha kumbukumbu nyuma na hatomaye fahamu zimamrudia. Akakumbuka kuwa alishawahi kumchora mpenzi wake tatoo kama hiyo miaka ya nyuma. Lulu alipoona Dastan, aliyekuwa mpenzi wa dada wa mpenzi wake Neron, akapanga kutoroka naye.

Mambo yalipokamilika, Lulu na Dastan walitoroka kutoka kwenye wodi ya vichaa na kwenda kuishi porini kwa muda.

Neron akiwa kwenye safari ya kumtembelea mapenzi wake Lulu na shemeji yake Dastan akiwa porini anamuona, msichana mmoja anakimbizwa na wahuni wakiwa na lengo la kumbaka. Neron an

amsaidia kwa kuwapiga vijana wake, lakini anapomuangalia sana msichana huyo haamini macho yake, kwani ni dada yake Nicol ambaye ilisemekana kuwa alifariki dunia na walishamzika.

Nicol anamwambia kaka yake kuwa hakufa, ila alipofika hospitalini alipatiwa matibabu na alipopata nafuu alitakiwa kueleza yote yaliyotokea na baada ya hapo, watu wa ustawi wa jamii walishauri akae mbali na familia yake kwanza, hivyo alipofika mzee Magari akaambiwa kuwa binti yake amefariki na akapewa maiti na msichana ambaye hakuwa na ndugu ili akazike.

Naron anamchukua dada yake na kumpeleka kwa mpenzi wake Dastan ambako pia Lulu yupo.

Hapo sasa kila mmoja akawa ana mpenzi wake, Dastan na Nicol, Neron na Lulu, huku wakihadithiana yote yaliyotokea nyuma hadi kujikuta wakiwa hapo.



# DRAKE KINARA 2019

## NYIMBO ZAKE ZASIKILIZWA DUNIANI KOTE

WAKATI tunakaribia mwaka 2020 , dunia inaendelea kupata watu waliotia fora katika nyanja mbalimbali ikiwamo upande wa burudani.

Kuna orodha kadhaa zimetajwa mbazo watu mbalimbali wamenga'ara kuongoza ndani ya mwaka 2019, moja ya eneo ambalo limeleta msisimko ni vibao vyenye ladha na kuleta furaha kwa wasikilizaji.

Katika orodha ya hivi karibuni, rapa Drake amejikuta akiwa kinara kati ya wanamuziki ambao muziki wake umesikilizwa zaidi duniani.

Katika utafiti huo uliofanywa na mtandao wa Spotify, wanamuziki huyo ameongoza kwa nyimbo zake kusikilizwa mara bilioni 28 duniani kote kuanzia mwaka 2010 hadi sasa.

Kutokana na orodha hiyo, Drake anakuwa rapa wa kwanza kusikilizwa na watu wengi tangu waanze kutoa nyimbo zao.

Wasanii wengine waliochomoza ni Ed Sheeran, Post Malone, Ariana Grande, Eminem.

Katika kipengele cha wimbo uliosikilizwa na watu wengi kibao cha 'Shape of you' ulioimbwa na Ed Sheeran umevunja rekodi kwa kusikilizwa na watu bilioni 2.4.

Nyimbo zingine zilizochukua nafasi ya pili hadi ya tano ni 'One Dance' Drake akishirikiana na Wizkidm na Kyla na 'Rock Star' wa Post Malone.




# Eti nini? Ugly hakuna atakayekuelewa

MWIGIZAJI wa filamu za ngono kutoka Nigeria, Uglygalz Mareme, amesema kutokana na kazi yake hiyo watu wanamtafsiri vibaya na kumuona kama mtu asiyefaa katika jamii.

Akuzungumza na mtandao wa Pulse, Uglygalz ambaye asilimia kubwa ya mwili wake umejaa michoro ya tatuu, amewasihi watu kutomchukulia kama yeye changudoa kwani nje ya kazi hiyo yupo tofauti.

"Mimi ni mchezaji wa filamu za ngono, nafanya kazi hiyo kwa ajili ya watu wenye umri mkubwa , lakini watu wananichukulia vibaya kama nipo pale kwa ajili ya pesa na wanasahau kuwa ninaigiza kwa lengo la kutoa burudani," amesema.



## Barna Boy, Davido waongoza kolabo 2019

WANAMUZIKI Barna Boy na Davido, wametajwa kama vinara wa wasanii waliotoa ngoma nyingi kwa kushirikiana na wengine katika ukanda wa kusini mwa jangwa na Lasaha na Afrika Kusini.

Kwa mujibu wa utafiti wa mtandao wa Apple Music uliochapishwa Novemba 3, 2019, umesema wasanii hao walioweza kuwashirikisha wanamuziki wengine kutoka nchi mbalimbali na nyimbo zao zilionekna kuwa bora.

Ukanda wa nchi hizo ni zilizo nje ya upande wa Kaskazini mwa Afrika pamoja na Comoros, Djibouti, Somalia na Mauritania. Nageria imetajwa kuwa ndiyo nchi pekee nyimbo zake zinapigwa sana.

## Carb B anapomkingia kifua mume wake asiumbuke

RAPA mkali wa Marekani, Cardi B, amemtetea mume wake akisema hawezi kuwajibika kutokana na ujumbe aliomtumia mpenzi wa mwanamuziki Tekashi 6ix9 ambaye yupo jela.

Cardi B ameibuka na kujaribu kuweka sawa tuhuma anazobebeshwa mume wake Offset akieleza kwamba akaunti yake ilishikiliwa na wadukuzi.

Kulingana na rapa huyo, Offset anajulikana kwa kazi zake na hawezi kufanya mambo hayo ya kiwendawazimu kwa kumuandikia ujumbe mchafu mwanamke huyo.





## Tacha kweli nyumbani pazuri

Anita Natacha Akide, maarufu kama Tacha, ambaye ameshiriki shindano la Big Brother Naija , amewasili nchini kwake Ghana na kupokelewa kishujaa.

Mshiriki huyo ambaye amekuwa maarufu katika mitandao ya kijamii kutokana na muonekano wake akiwa ndani ya nyumba hiyo, alitolewa baada ya kukwaruzana na mshiriki mwenzake Mercy na kutoleana maneno yasiyofaa.

Mama yake Tacha ambaye sasa ni marehemu alikuwa anatoka Ghana na huko ndipo alikuwa na mashabiki wengi wakiwamo mastaa wa nchi hiyo Moesha Boduong na Afia Schwarzenegger.

## Wizkid ang'ara Twitter 2019

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Wizkid amepewa tuzo maalum baada ya kuongoza kuwa na wafuasi wengi kuliko wasanii wote nchini humo.

Mtumiaji maarufu wa mtandao huo, Joey Akan, alimkabidhi tuzo hiyo na kumtaja kama mtu aliyevunja rekodi kipindi cha muongo mmoja.

Kulingana na Joey, Wizkid amekuwa akitumia mtandao huo kwa miaka 10 sasa na Nigeria inajivunia kuwa na mtu mwenye kipaji na juhudi ya kazi yake.



**SAFU**



Na John Juma
0716217615

## MIONZI YA SHERIA

# Kukabiliana na wanaouza mali shauri likiwa kortini

INAWEZEKANA umefungua shauri la ndoa, au una maombi ya talaka, mgawanyo wa mali ,malezi ya watoto au vyote.

Wakati huo ambao kesi haijaanza, au imeanza kusikilizwa lakini haijaisha, unahisi au unaona mali za ndoa ambazo pengine zinatakiwa kugawanywa zikiwa katika hatari ya kuuzwa, kugawiwa, kuharibiwa au kubadilishwa umiliki. Unaona bayana kuwa shauri litakapomalizika patakuwa hakuna kitu au kitakacho kuwepo ni kidogo.

Unajihoji nini ufanye kisheria katika mazingira kama haya ili kuokoa mali hizi, ili usije kukosa haki yako kesi itakapokwisha? Hiki ndicho kitakachozungumzwa hapa na safu hii ya mionzi ya sheria.

Kitu unachotakiwa kufanya kimeelezwa katika kifungu cha 138( 1 ) cha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Kifungu kinasema pale ambapo mtu ataona kuna hatari ya mali kuuzwa, kuharibiwa au kupotezwa kwa namna yoyote ile basi atakuwa na haki ya kuomba mahakama itoe zuio la muda kumzuia mtu yeyote kuiuza, kuibadili umiliki, kuiharibu, kutoa zawadi au kufanya kitu kingine chochote chenye lengo la kuathiri mali hizo.

Kitu hiki pia kimeelezwa mara nyingi na Mahakama Kuu pamoja na Mahakama ya Rufani katika kesi mbalimbali mojawapo ikiwa ni hii ya Elizabeth Gikene Vs John Zakharia Gikene shauri la Ndoa Namba 5/2004.

Kwa hiyo utakachofanya, kwanza kama kesi iko mahakama ya wilaya, ya hakimu mkazi, au mahakama kuu na unaye wakili anayekuwakilisha cha kwanza ni kumwambia kuhusu huo wasiwasi wako wa dalili za kupotezwa kwa mali lakini pia muombe mfanye utaratibu wa zuio hili. Bila shaka mtakubaliana kuhusu hilo.

Pili, kama shauri liko katika mahakama zilizotajwa hapo juu lakini hauna wakili anayekuwakilisha ni muhimu kumtafuta wakili yeyote umweleze wasiwasi wako na kumuomba akuandalie maombi ya zuio hili ili uzuie mali wakati shauri la msingi likisubiriwa kuisha. Mtaelewana kuhusu hili na mtafanya kama mlivyoelewana.

Maombi haya ni lazima kumtafuta wakili hata wa kukuandikia tu halafu wewe ukaenda mwenyewe mahakamani, kwasababu mtu ambaye sio Wakili sio rahisi kuandaa maombi haya.

Zaidi, kama kesi iko mahakama ya mwanzo hapo hukuna haja ya wakili kuandaliwa maombi rasmi bali ni kumweleza hakimu anayesikiliza shauri lako kwa mdomo kuhusu wasiwasi wako wa mali kuharibiwa na utamuomba atoe zuio la muda mali zisiguswe mpaka shauri la msingi liishe.

**Zaidi, kama kesi iko mahakama ya mwanzo hapo hukuna haja ya wakili kuandaliwa maombi rasmi bali ni kumweleza hakimu anayesikiliza shauri lako kwa mdomo kuhusu wasiwasi wako wa mali kuharibiwa na utamuomba atoe zuio la muda mali zisiguswe mpaka shauri la msingi liishe.**

Kama utaweza kumtajia hata kifungu cha sheria kilichoelezwa na Makala hii au pamoja na hiyo kesi iliyotajwa ya Gikene ambavyo kwa pamoja vinaruhusu maombi haya ya zuio.

Kama utashindwa kufanya hivyo ni vyema kumwabia hakimu bila kumtajia kifungu, atatoa msaada.

Mara nyingi tatizo hili la kuharibiwa mali wakati shauri likiendelea mahakamani limekuwa likiwakumba zaidi kinamama.

Anapofungua shauri kuomba talaka au mgawanyo wa mali basi mwanaume huanza kuuza baadhi ya mali au kuzibadilisha umiliki ili wakati shauri linaisha mali ziwe zimeisha ili mwanamke asiambulie kitu, au kwa lengo kuwa ikifikia ushahidi kila mali itakayotajwa na mwanamke kuwa ni ya ndoa akatae kuwa sio yake au ilishauzwa.

Hata wanaume nao hukumbwa na tatizo hili lakini zaidi ni wanawake. Basi hili lisikupe tabu tena kwa kuwa dawa yake ndiyo hiyo.

Na kwa taarifa tu, mali ikizuiliwa na mahakama isiuzwe na mtu akaendelea na uuzaji au kuiharibu adhabu yake ni kifungo cha miezi sita jela kwa kuidharau mahakama.

Lakini pia yule aliyenunua anakuwa amepoteza hela yake kwakuwa amenunua mali ambayo imezuiwa na mahakama na hivyo ni batili. Basi ni vyema kuchukua hatua na kulinda haki na mali kwa mujibu wa sheria.



Na Reubeni Lumbagala

## KALAMU YA MWALIMU

# Taifa linahitaji midahalo kukuza uelewa na udadisi

MIDAHALO ni jukwaa muhimu kwa wanafunzi wa ngazi zote za elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu kujifunza mengi katika misingi ya kujenga hoja na mifano kuntu ya mada zinazojadiliwa.

Suala la midahalo katika taasisi nyingi za elimu nchini halijapewa kipaumbele kama nyenzo muhimu kwa wanafunzi kujifunza na kukuza uelewa na udadisi wa masuala ya kimasomo, kijamii, kiuchumi na kisiasa pia.

Upo umuhimu sasa wa midahalo kupewa kipaumbele ili wanafunzi waweze kukuza uelewa na udadisi kupitia mawazo kutoka kwa wanafunzi wenyewe.

Kabla ya mdahalo kufanyika ni lazima ichaguliwe mada ya kujadiliwa. Pili wanafunzi wapewe muda wa kutafuta mawazo kuhusiana na mada husika ya mjadala.

Makundi mawili yanayounga mkono mada na yanayopinga mada ni lazima yapatikane ili siku ya mjadala, makundi mawili kinzani yapatikane tayari kwa mdahalo.

Shule ambazo zinatilia mkazo midahalo shuleni ni lazima zitakuwa na nafasi kubwa ya kufanya vizuri katika mitihani. Mada zinazojadiliwa katika midahalo huwa ni sehemu ya mada zilizopo katika mitaala ya elimu, hivyo wanafunzi wanapowekewa utaratibu wa kufanya midahalo shuleni na vyuoni ni sehemu ya wanafunzi kuongeza maarifa katika yale waliyojifunza darasani na kuwajengea kujiamini.

Ni jambo la msingi sana kwa mhitimu kujiamini na kusimama mbele ya watu kutoa mawazo yake kwa kujenga hoja madhubuti.

Sehemu muhimu ya mwanafunzi kujenga kujiamini ni katika kushiriki midahalo. Hivyo mwanafunzi ambaye anashiriki kikamilifu katika midahalo ana nafasi kubwa ya kujiongezea maarifa na kujiamini na hivyo kuwa mhitimu bora anayekubalika katika soko la ajira kwa kujiajiri au kuajiriwa.

Shule ya Kimataifa ya Feza kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kwa kutambua umuhimu wa midahalo kwa wanafunzi, imeweka utaratibu kila mwaka kuwa na mashindano ya midahalo kwa wanafunzi wa shule za serikali na shule binafsi nchini wakipambanishwa na wanafunzi wengine kutoka nchi nane za Afrika ikiwamo Kenya na Zimbabwe.

Mashindano hayo ya kimasomo yanajulikana kama Africa Open Schools Debate Championships, yamesaidia kuwajengea wanafunzi uelewa, udadisi na kujiamini zaidi. Midahalo hiyo huwawezesha wanafunzi kuelewa masuala mbalimbali ya masomo na kuwapa mbinu za kujiamini mbele za watu na kuzungumza hadharani.

Katika ratiba za masomo shuleni ni muhimu suala la midahalo likapewa kipaumbele. Midahalo inaweza kufanyika siku yeyote kulingana na nafasi yao ya shule katika kulitekeleza jambo hili.

Wanafunzi waelimishwe umuhimu wa ushiriki wao katika midahalo kwa mustakabali mwema wa masomo na maisha yao ya sasa na ya baadae.

Ili suala la midahalo shuleni liwe endelevu na lipate ushawishi kwa wanafunzi ni lazima walimu wote washirikiane katika kushiriki na kusimamia midadalo hiyo. Kama mdahalo utaitishwa lakini walimu wakashindwa kufika na kushiriki, wanafunzi watakosa hamasa ya kuendelea kushiriki midahalo mengine.

Timu ya walimu iweke mikakati kuhakikisha walimu wanashiriki wote ili programu hiyo iwe endelevu. Mathalani, mwalimu au walimu wa zamu katika juma ambalo mdahalo unafanyika kwa kushirikiana na walimu wengine wanapaswa kushiriki na kuusimamia mdahalo huo. Walimu wawe waamuzi wa kutoa alama kwa washiriki ili mwisho wa mdahalo upatikane upande ulioshinda na upande ulioshindwa.

Kutokana na wanafunzi kukosa uelewa wa kanuni za midahalo, walimu watoe miongozo muhimu inayoongoza majadiliano hayo.

Katika mdahalo, walimu wazingatie washiriki wanaotoa hoja kwa mifano kuntu kama njia ya kupata alama nyingi katika mjadala huo. Katika shule za sekondari, lugha inayotumika katika midahalo ni Kiingereza.

Ushiriki wa wanafunzi katika midahalo ni njia bora ya wanafunzi kukuza uelewa na umahiri katika lugha ya Kiingereza ambayo inatumika katika masomo yote ya sekondari isipokuwa Kiswahili pekee.

Matumizi ya Kiingereza katika midahalo inachangia sana kuwajengea uwezo wanafunzi katika kuzungumza Kiingereza kwa ufasaha lugha ambayo kwa baadhi ya wanafunzi wengi wa sekondari ni tatizo kubwa na kuchangia kufeli kwao katika mitihani.

Kabla ya siku yenyewe ya mdahalo wanafunzi hupata nafasi ya kuandaa mawazo ambayo watayawasilisha katika siku yenyewe ya mdahalo.

Mwanafunzi anaweza kutumia kamusi kutafuta misamiati ya Kiingereza ambayo anadhani anaweza kuitumia siku ya mdahalo na hatimaye kukuza uelewa wa lugha hiyo ya kimataifa ambayo popote duniani ndiyo kiungo cha mawasiliano.

Midahalo ikitumika kikamilifu ni njia bora ya kuwaandaa na kupata wahitimu bora. Midahalo ipewe kipaumbele mashuleni. Tafakari.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Maoni: 0764 666349.**

MAKALA

# MAAJABU MAABARA MKEMIA MKUU

# Kufanikisha tiba kan kutibu figo, yachamb

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), iliyoanzishwa takribani miaka 124 iliyopita wakati wa ukoloni wa Kijerumani, kuna baadhi ya watu wanaoichukulia kama taasisi inayojishughulisha na kuchunguza masuala ya dawa pengine na kemilikali na hata sumu.

Wanaitizama kama mamlaka inayojielekeza zaidi katika masuala ya viwandani na udhibiti kemikali, lakini ukweli ni kwamba ni moja ya taasisi nyeti nchini inayofanya kazi nyingi na za kitaalamu zinazogusa moja kwa moja maisha ya watu iwe vijijini au mjini na kutoa majibu, ufumbuzi na mwelekeo mpya wa kutatua changamoto.

Hivi karibuni Mkemia Mkuu wa Serikali Dk. Fidelice Mafumiko, anazungumza na wanahabari kuhusu utendaji kazi wa maabara hiyo katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano. Anagusia masuala mengi yakiwamo mafanikio, mapato na tiba.

### TIBA YA FIGO

Dokta Mafumiko akianza na eneo la matibabu anasema maabara hiyo inashirikiana na wataalamu wa afya kwenye kufanikisha matibabu ya figo.

Anasema mamlaka inashirikiana na taasisi za tiba kama Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, ya Rufani ya Kilimanjaro (KCMC) na Bugando, kufanya uchunguzi wa kimaabara kwa kutumia teknolojia ya vinasaba vya binadamu kwenye uchunguzi wa kutambua uhusiano wa mtoaji na mpokeaji wa figo.

Mchakato huo ni wa kuwezesha utoaji na upandikizaji wa figo kutoka kwa anayechangia na kuipanda kwa mgonjwa kwa mafanikio.

Pia, maabara imefanya uchunguzi wa kuwezesha utambuzi wa jinsi tawala (dominant gene) kwa watoto wanaozaliwa na jinsi mbili ya kike na ya kiume ili kupata matibabu stahiki.

"Katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imechunguza na kulinganisha kwa ajili ya upandikizaji wa figo kwa watu 29 na utambuzi wa jinsi tawala 48." Anasema.

### KUBORESHA TIBA

Licha ya kwamba ni mipango ya baadaye, Mkemia Mkuu wa Serikali anasema mamlaka hiyo inaendelea kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha mahusiano na taasisi zinazotoa huduma za afya hasa katika matibabu ya kisasa yanayohusisha tiba ya jine "gene therapy", matibabu ya figo, utambuzi wa jinsi tawala (sex ambiguity).

### KUTIBU KANSA

Dokta Mafumiko anasema mamlaka itaendeleza ushirikiano na Hospitali ya Muhimbili na nyingine katika kuwawezesha wagonjwa wenye matatizo mbalimbali ikiwamo saratani ya damu na tiba ili kutibiwa kwa utaratibu wa kupandikizwa uboho au kufanyiwa 'bone marrow transplant'

Uboho ambao ni urojo unaokaa katikati ya mifupa ndiyo unaohusika na kuzalisha seli kuu au seli mzizi (stem cells) pia huzalisha seli nyekundu. Iwapo mtu anapata saratani ya damu urojo au kiwanda hicho cha kuzalisha seli huharibiwa na mwili kukosa damu.

"Ili kuendelea kufuatilia maendeleo ya wagonjwa baada ya tiba hii, watahitajika kufanyiwa uchunguzi wa vinasaba hususani 'chimerism'ambao ni utaalamu wa kuangalia iwapo kuna vinasaba vya ina tofauti, hilo hufanyika kwa ajili ya kubaini hali halisi na kufanikisha kupandikiza vinasaba vipya.

Aidha, anasema vifaa vya kisasa na wataalam waliopo kwenye mamlaka itaimarisha ushirikiano na taasisi za kitaaluma mbalimbali ili kufanya utafiti unaohusiana na uchunguzi wa vinasaba vya binadamu kwa mfano selimundu 'sickle cell, kisukari, saratani na 'population genetics'.

Anasema utafiti huo ukifanyika utaokoa fedha za umma ambazo zingetumika kwa sampuli kupelekwa nje ya nchi kwa ajili ya uchunguzi.

### UTAMBUZI VINASABA

Mkemia Mkuu wa Serikali anasema mamlaka inashiriki katika kutoa majibu ya maswali kwenye majanga makubwa na uwezo wa utambuzi wa miili iliyoharibika likiwamo tukio la kuzama kwa MV Nyerere wilayani Ukerewe mkoani Mwanza mwaka 2018 na katika hilo miili 10 ilifanyiwa uchunguzi.

Anasema miili yote ilitambuliwa baada ya kufanya ulinganifu wa ndugu 12 katika sampuli 39 zilizochunguzwa.

Dokta Mafumiko anasema ajali nyingine ya gari la abiria iliyotokea Tarime mkoani Mara mwaka 2018, walichukua sampuli ya miili 14 yote ilitambuliwa baada ya ndugu 25 kufanyiwa uchunguzi wa vinasaba.

Anasema ajali ya tangi la mafuta iliyotokea Morogoro, Agosti 10, mwaka huu na miili 69 ilifanyiwa uchunguzi na 61 alitambuliwa kulingana na sampuli za ndugu waliojitokeza na kukabidhiwa mabaki.

Anazungumzia ajali nyingine ya lori lililowaka moto Kibiti mkoani Pwani mwaka huu, watu watano walichukuliwa sampuli na watatu walitambuliwa baada ya ndugu kujitokeza.

### KANZIDATA DNA

Aidha, Mkemia Mkuu anasema GCLA ipo katika hatua za awali katika uanzishwaji wa Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma zikiwamo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida )na Wakala wa Usajili wa Vifo na Uzazi (Rita).

Anasema wataalam kutoka katika taasisi hizo muhimu wameshirikishwa katika hatua za awali za uanzishwaji wa kanzidata ya taifa hususani utayarishaji wa andiko dhana la uanzishwaji wake.

Aidha, kwa kuzingatia ushauri wa wataalam katika andiko la uanzishwaji wa Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu, mamlaka inakusudia kuanza kuingiza taarifa hizo katika mfumo maalum.

Anasema kwa kuwa taarifa hizi kuwa zinahitajika katika utambuzi wa binadamu kwa ajili ya utatatuzi wa changamoto mbalimbali ikiwamo uchunguzi wa makosa ya jinai kama vile ubakaji, wizi, mauaji, majanga na masuala ya kijamii yakiwamo mirathi, uhalali wa mzazi kwa mtoto.

### MAFANIKIO

Kuhusu mafanikio Mkemia Mkuu wa Serikali anasema, wamewekeza katika miundombinu ya maabara za uchunguzi, vifaa kama mitambo na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama).

Anasema wamefanya usajili wa wadau wa kemikali kwa njia ya mfumo wa kielektroniki (portal) ulioanza April Mosi, mwaka huu, mamlaka imesajili wadau 1,148 kati ya 2,500 na kutoa vibali 1,894 kwa njia ya mtandao hadi sasa.

Ongezeko hilo pia limesogeza huduma karibu zaidi na wananchi kupitia ofisi za kanda na mipakani.

Dokta Mafumiko anasema katika kipindi cha miaka minne mamlaka imeongeza kanda moja na kuweka wakaguzi katika mipaka mikubwa saba ya Tarakea, Horohoro, Tanga Bandarini, Kasumulu, Kabanga, Rusumo na Kigoma-



Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali . **PICHA ZOTE: MAABA RA YA MKEMIA.**




Mkemia Mkuu, Dk Mafumiko (kushoto) akiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Profesa Esther Hellen Jason.

# sa ya damu, kiungo bua DNA ajali zote



Manyovu.

Kadhalika wakala umeimarisha usimamizi na udhibiti wa kemikali kwa lengo la kulinda afya za wananchi na mazingira dhidi ya matumizi yasiyo salama ya kemikali.

Anasema mamlaka ikiwa ni mtekelezaji wa Sheria ya Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sheria namba 3 ya mwaka 2003, inasimamia uingizaji, utumiaji, usambazaji na usafirishaji wa kemikali ambazo ni malighafi za kutengeneza bidhaa mbalimbali viwandani.

Anasema lengo ni kuwezesha na kuchangia jitihada za serikali ya awamu ya tano kuelekea uchumi wa Viwanda ifikapo 2025.

Dokta Mafumiko anasema, mamlaka kupitia Waziri wa Fedha na Mipango imefuta jumla ya tozo 17 na kupunguza tozo 8 katika utekelezaji wa Sheria ya Kemikali.

"Hali hii imewezesha kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini kwa kupunguza mzigo wa gharama kwa wafanyabiashara wa kemikali katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali," anasema Mkemia Mkuu.

Anasema mamlaka imefanya pia marekebisho ya Sheria ya Kemikali za Viwandani na Majumbani namba 3 ya mwaka 2003 kwa kufanya maboresho ya kifungu cha 43(11) ili kuruhusu uingizaji wa kemikali katika ujazo mkubwa usiokuwa kwenye vifungashio.

Marekebisho hayo yanatarajiwa kuongeza wingi wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam, Tanga au Mtwara kutegemeana na ipi itakuwa inatekeleza jukumu hilo na hivyo kukuza biashara na kuongeza mapato.

Anasema maabara hiyo imeimarisha kutoa mafunzo na elimu kwa wadau wa mamlaka hiyo na mwaka 2015/16 walitoa kwa watu 2,644 na mwaka 2017/18 walitoa kwa watu 11,598.

Anaeleza kuwa ongezeko hilo linatokana na kuimarisha eneo la mafunzo kwa wadau, mfano, wanaojishughulisha na kemikali, jeshi la polisi, madaktari, wanasheria, wachimbaji wa madini.

Anaeleza kuwa, idadi hiyo imefikiwa kupitia njia mbalimbali ambazo zinatumika kutoa mafunzo ikiwamo kujitangaza kupitia vyombo vya habari, ushiriki katika maonyesho mbalimbali na makongamano.

"Lengo la kuufahamisha umma majukumu ya mamlaka na namna watakavyofaidika na huduma za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali," anasema Dk. Mafumiko.

**KUONGEZA MAPATO**

Mkemia Mkuu anasema mapato ya mamlaka hiyo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 9.342 mwaka 2015/16 hadi sasa yamefikia bilioni 24.246 sawa na ongezeko la asilimia 118.

Anasema mapato hayo yameongezeka kutokana na kuimarishwa kwa mifumo ya udhibiti na ukusanyaji wa mapato kupitia mifumo ya Epicor na GePG na kuimarika kwa mifumo ya ndani ya ukaguzi na udhibiti fedha kuimarika kwa utunzaji wa hesabu.

Dk. Mafumiko anasema fedha hizi zimetumika kwenye ununuzi na ukarabati wa mitambo ya maabara, kuboresha miundombinu ya maabara, kununua vitendanishi na kuimarisha ukaguzi wa kemikali.

**HISTORIA**

Mamlaka hiyo ilianza mwaka 1895 ikijulikana kama "Maabara Kuu ya Kemia" wakati wa enzi za utawala wa Wajerumani.

Lengo kuu la kuanzishwa kwake wakati huo lilikuwa ni kufanya utafiti wa magonjwa ya ukanda wa joto ikiwa ni pamoja na malaria na kifua kikuu (TB).

Baada ya Uhuru mwaka 1961 Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilikuwa Idara ndani ya Wizara ya Afya na baadaye ikawa wakala mwaka 1999 kwa Sheria ya Wakala za Serikali namba 30 ya mwaka 1997.

Kwa sasa taasisi hiyo inajulikana kama Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutokana kuundwa rasmi kisheria kupitia Sheria ya Serikali namba 8 ya mwaka 2016. Mkemia Mkuu anawaeleza wanahabari kuwa majukumu makuu ya mamlaka yamebadilika si kuchunguza magonjwa kama TB wala malaria, bali yamegawanyika katika maeneo makubwa matatu ambayo ni pamoja na kufanya uchunguzi wa kitaalam.

Anautaja uchunguzi wa kisayansi na kimaabara wa sampuli na vielelezo mbalimbali kama vile vinavyotokana na makosa ya jinai, usalama na ubora wa bidhaa za masuala ya kijamii na usalama wa afya kazini.

Dokta Mafumiko anasema pia mamlaka inasimamia utekelezaji wa sheria tatu ambazo ni za Usimamizi na Udhibiti wa Kemikalai za Viwandani na Majumbani.

Aidha, husimamia na kudhibiti matumizi ya vinasaba vya binadamu na kutoa ushahidi wa kitaalam mahakamani kwenye mashauri yote yanayohusisha matokeo ya uchunguzi wa kimaabara.

"Lengo ni kuchangia katika kuleta haki, amani, utulivu wa nchi na utawala bora kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali namba 8 ya 2016 na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura namba 20," anasema Dk. Mafumiko.



Rais John Magufuli akipata maelezo kutoka kwa Zacharia Ng'weshemi, kuhusu uendeshaji wa mashine ya kisasa ya uchunguzi yenye uwezo wa kugundua aina mbalimbali za dawa za kulevya, madini tembo na sumu, alipotembelea Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Agosti 20, 2019. Mashine za aina hiyo kwa Afrika zipo Tanzania, Afrika Kusini na Mauritius .

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 23 00)



Dondoo: Kulia

1. Kiev ni mji wake mkuu
5. Mji mkuu wa Saudi Arabia
6. Kutiwa doa
10.Potea kwa muda
13.fikisha maneno ya salamu
15.Soni
16. Kiongozi wa sala msikitini
19.Chuma, shaba, bati, fedha
23.fikicha
24.Mnyama mkubwa kama Paka
25.Nyumba za ibada
26.Ushuru
28.Hapana
29.Kaa imara

Dondoo: Chini

1. Utoaji huduma kwa jinsia
2. Kahaba wa Yeriko
3. Wingi wa neno ulimi
4. Sura, mlango
5. Tamasha la urafiki Asia
7. Mke wa Raila Odinga
8. Kanusha au batilisha haki
9. Mji mkuu wa Rwanda
11.Fedhehesha
12.Shutumu
14.Kitu chenye kudhuru
17.Mapatano 18.Uhasama
19.Jiji kubwa kuliko yote India
20.Pengine 21.Mji mkuu Senegal
22.Chukia 26.Ongezeka kimo
27.Sala

## Jibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | L | A | Y | S | I | A | | M | | K | |
| U | | O | | | | | | S | A | N | A | A |
| Z | A | N | Z | I | B | A | R | | J | | T | |
| I | | D | | N | | N | A | N | A | S | I | |
| K | I | O | N | G | O | Z | I | | R | | | M |
| I | | N | I | A | B | A | | | I | | | T |
| | T | | A | W | A | | T | A | B | I | B | U |
| S | H | E | M | A | S | I | | | I | | | N |
| | A | | E | | A | G | I | Z | O | | | G |
| | B | A | Y | A | N | A | | I | | M | | I |
| | I | | | | J | | T | A | M | B | I | |
| M | T | A | M | B | O | | | D | | W | | |
| | I | | | | | D | H | A | M | A | N | A |

SIKU 16 KUPINGA UKATILI

# Wanaume hunyanyaswa kuitwa 'mwanaume suruali ni GBV'

**Na Gaudensia** Mngumi



Mwanamume akipata kichapo mtaani. Kinababa watasema hawapigwi na GBV haiwahusu? **PICHA: MTANDAO**

SIKU 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ambayo ni kampeni ya dunia ya kuwalinda wanyonge hasa wanawake, watoto, wahitaji na wengine ili wasionewe, inakumbusha watu kujiepusha na ukatili na unyanyasaji kijinsia (GBV).

Kampeni hiyo ya GBV -Gender Based Violence iliyoanza tangu wiki iliyopita na inayotarajiwa kufikia kilele Jumanne ijayo Desemba 10, mara nyingi wanaume wanaipuuza na kudhani kuwa wanaonyanyasika ni wanawake na kwamba wao mambo hayo hayawahusu.

Kwa ujumla unyanyasaji wa kijinsia unawaumiza wote. Kila mmoja kwenye jamii anaumia bila kujali jinsi yake iwapo ni mwanamume au mwanamke , japo ukatili unaohusisha kubakwa, kulawitiwa, kunajisi watoto, kutukanwa, kupigwa, kukeketwa, mimba na ndoa za utotoni, kupigwa na wenza katika ndoa, kulazimishwa kuacha kazi na pia kutelekezwa kunawaumiza zaidi wanawake kuliko wanaume.

Hii ni kwa sababu wanawake ndiyo wanaobeba mzigo mkubwa wa majukumu ya kifamilia na ukatili unapotokea unakuwa ni dhamana ya mama kuupokea na kushughulikia mateso hayo.

Mathalani, binti akibakwa mama anahangaika naye kuanzia kumfikisha polisi, hospitalini, kumtibu kama ameambukizwa maradhi, kumlea na mtoto iwapo amepata ujauzito na mwisho kumsaidia kwa kila hali ili apate mtoto na kuendeleza maisha.

Wakati huo baba anaweza kuwatukana mama na binti kwa matusi ya nguoni na kashfa dhidi ya tukio hilo na vyote hivyo ni unyanyasaji.

**WANAUME WAHUSIKE.**

Mara nyingi kwenye harakati za siku 16 za kupinga ukatili, wanaume hawapendi kuhusika moja kwa moja. Wapo wengine wanasema hawanyanyasiki lakini ukweli ni kwamba hata wao wamo.

Kwa mfano, wiki hii wakati Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam Lazaro Mambosasa, anapozungumzia Siku 16 za kupinga unyanyasaji, anawakumbusha wanaume kuwa hata wao ni waathirika watumie madawati ya jinsia kueleza kinachowasibu.

"Nanyi wanaume mlio katika uhusiano ikitokea mmefanyiwa ukatili na mwenza wenu msisite kutoa taarifa," anawahimiza Mambosasa.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, anawataka wanaume kujitokeza kwani hata wao kampeni hizo zinawahusu na wanaumizwa na GBV kwa kiwango kikubwa.

Anawaambia kuwa wanaume wanapigwa, kutukanwa na kunyanyaswa na wanawake wao, lakini wanakaa kimya na mwisho hukimbia familia na kuwaacha watoto wakiathirika zaidi.

"Kama mtaogopa kwenda kwenye madawati ya jinsia polisi kwa kuwa mnaogopa wanaosikiliza malalamiko hayo ni wanawake njooni hata kwetu sisi viongozi ,"anasema Msafiri.

Pia, Mwakilishi wa Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto, kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Dar es Salaam, Faiza Suleiman, anapozungumzia suala la ukatili wa kijinsia anasema ingawa jamii inaamini kwamba ukatili wanafanyiwa wanawake , wanaume nao ni waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili, lakini wamekuwa wakijificha.

"Tatizo ni mfumo dume kwamba mwanamume hawezi kupigwa au kunyafiwa ukatili na mwanamke, lakini ukweli ni kwamba wapo tena wengi. Ushauri wangu ni kwamba wanaume hebu fungukeni," anasema Suleiman.

Pamoja na ushauri wa viongozi hao, ni vyema jamii kufahamu kuwa unyanyasaji wa wanaume unafanywa kwa njia nyingi, lakini hata kwa maneno na mara nyingi kuwasema , kuwalaumu muda wote na kuwa na gubu lisilokwisha ndani ya nyumba ni GBV.

Wapo baadhi ya wanawake wanawaambia waume au wapenzi wao wewe ni mwanamume suruali'. Maneno kama hayo ni unyanyasaji kijinsia na husababisha wanaume wengine kujinyonga au kukimbia familia zao.

Kumwambia mwanamume tena mbele za watu au watoto kuwa wewe huna kitu ni au kumkejeli mwenza kuwa ni 'mwanamume jina'ni kuwaumiza wanaume kisaikolojia na kimwili.

Maneno kama mume bwege ,mume kivuli,' 'wanaume wakiitwa utakwenda'ni matusi ambayo hata wanaume hayawafurahishi kwa namna yoyote.

**KUSIFIWA KUNYANYASA**

Kuna baadhi ya jamii ambazo wanawake husifika katika kunyanyasa wanaume. Hili si jambo la kufurahisha kuwa 'ninyi'watu fulani ni mabingwa wa matusi, kusuta na kudhalilisha wanaume, kumbukeni kuwa huo ni unyanyasaji na udhalilishaji na wiki hii mnakumbushwa kuuacha.

Jamii ikumbuke kuwa hakuna anayefurahia kufokewa muda wote, kuhojiwa na hata kupuuzwa kila anapofika nyumbani kwake.

Kwa mfano wapo kinamama ambao muda wote kama atapiga simu kwa mwenza na akachelewa kuipokea au asiipokee anaanzisha ugomvi.

Maswali kama mbona hupokei simu yangu lakini ya nyumba ndogo huchelewi kuipokea ndiyo anayokutana nayo baba watoto wako.

Wapo pia baadhi ya wanawake wanapenda kupekua simu za waume zao na kuwauliza mbona hii namba unaipiga sana kuna nini? Au ni nina mwenzangu?

Kuna maneno mengine matusi ambayo huambatana na wanaume wenye kipato kidogo ni pamoja na kukutana na kauli za kuudhi muda wote.

Wakifika nyumbani wanaanza kusalimiwa na maneno ya kashfa kama 'mwanamume pesa'au 'kama mtu huna nyumba, gari wala mali ni kama umekufa.'

**WATOTO HUTUMIKA.**

Baadhi ya wanaume katika soko la Tandale, jijini Dar es Salaam, wanaozungumza na Nipashe kuhusu siku 16 za kupinga ukatili wanasema wanawake huwatumia watoto kuwatukana baba zao (waume wao) pale wanapoona kuwa hawana kitu, "Kwa ukali mama anasema nyie mnanililia mnataka chakula kamwambieni baba yenu muulizeni kwanini hana hela . " Nani kamwambia awe maskini' anasema Albogasti Mushi, anayeuza matunda katika soko hilo.

Mushi anasema wakati mwingine mwanamume anaondoka au anarudi usiku wa manane na kuondoka mapema kwenda kijiweni ili awe na amani.

"Tunatukanwa na watoto na mama zao ndiyo maana tunaamua kuondoka na kuwaambia watakula matusi yao. Tutafanya nini sasa. Lakini ukiondoka mwanamke anakugeuzia kibao kuwa unamnyanyasa na umeitelekeza familia na watoto"anasema Mushi.

Kwa hiyo ni vyema kufunguka na kueleza matatizo ili kupata ushauri nasaha lakini pia jamii ijue kuwa unyanyasaji unamhusu kila mtu.

# Gavana wa Nairobi mbaroni kwa ufisadi

**NAIROBI, Kenya**

MIKE Sonko, Gavana wa Jimbo Nairobi amekamatwa na polisi kwa tuhuma za ufisadi.

Tukuo hilo linatokea baada ya mkurugenzi wa mashtaka ya umma nchini Kenya, Nurdin Hajj, kutoa agizo la kukamatwa kwake kwa madai ya kuhusika kutoweka kwa Dola milioni 3.5 za umma.

Gavana Sonko ni wa tatu kwa magavana waliopo madarakani kushitakiwa kwa tuhuma za ufisadi.

Sonko alikamatwa Ijumaa wiki hii katika mji wa Voi ulioko kwenye pwani ya Kenya saa kadhaa baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, kusema kuwa ana ushahidi wa kutosha kumfungulia mashitaka mwanasiasa huyo.

Mbunge huyo ambaye ni tajiri anatuhumiwa kwa kutoa zabuni kwa washirika wake wa karibu, kugushi nyaraka na ubadhirifu wa wa fedha za jimbo la Nairobi.

Mkurugenzi huyo mkuu wa mashitaka ya umma pia alieelezea wasiwasi wake kuhusu madai ya gavana huyu kuingilia kati uchunguzi kwa kujaribu kuficha ushahidi.

Awali Sonko aliwasilisha kesi mahakamani kuomba uchunguzi dhidi yake ukomeshwe lakini kesi hiyo ilitupiliwa mbali.

Gavana huyo pia alidaiwa kukabiliwa na tuhuma za ulanguzi wa dawa za kulevya na utakatishaji wa fedha.

Hivi karibuni mamlaka ya magereza ilimtuhumu kwa kutoroka jela miaka 20 iliyopita.

*BBC*



Gavana Sonko akihutubia wananchi katika mkutano kisiasa .**PICHA: TANDAO**

# Ghorofa laporomoka kuua, kujeruhi kadha

**NAIROBI, Kenya**

WATU wawili wamethibitika kuwa wamefariki dunia baada ya jengo la ghorofa sita kuanguka jana asubuhi katika eneo la Embakasi jijini Nairobi.

Pamoja na vifo hivyo wengine kadhaa wanahofiwa kuwa wamenaswa chini ya kifusi cha jengo hilo.

Kazi za uokoaji zinaendelea na ripoti zilisema kuwa watu kadhaa wameokolewa na kukimbizwa hospitalini.

Watu watatu wakiwa na majeraha makubwa walitolewa kutoka kwenye kifusi na kupelekwa kwenye hospitali ya rufani ya Kenyatta, jijini Nairobi, wakiwamo mama na mtoto.

Familia 46 zilikuwa zikiishi kwenye jengo hilo.

Polisi na jumuiya ya Msalaba Mwekundu kutoka kaunti ya Nairobi wako kwenye eneo la tukio.

Hata hivyo walipata wakati mgumu kudhibiti kundi kubwa la watu waliojitokeza kushuhudia mkasa huo.

Shughuli za kuwaokoa walionasa kwenye jumba hilo zinaendelea huku magari ya kubeba wagonjwa yakiwa yamefika kutoa msaada wa dharura.

Mkuu wa Polisi Philip Ndolo alisema kuwa wanafanya kila wawezalo kuwaokoa watu waliokwama.

Haikufahamika sababu za jengo hilo kuporomoka na ni watu wangapi wamekwama kwenye jengo hilo.Wenyeji wanadai kuwa huenda ikawa watu wengi wamekwama kwani jengo lenyewe liliporomoka mapema asubuhi na wakati huu shule zikiwa zimefungwa.

Wenyeji wanailaumu Idara ya Mipango ya Ujenzi nchini kwa kutohakikisha majengo yaliyojengwa ni salama kutumika.Walidai kuwa Idara hiyo imezembea katika kukagua usalama wa majengo hasa jijini Nairobi na hivyo kuwaacha watu katika hatari ya kuumizwa na maghorofa yanayoanguka.

Hili si jengo la kwanza kuporomoka. Mwezi Septemba mwaka huu ghorofa moja inayomilikuwa na shule eno la Dogoretti Nairobi iliporomoka na kuwaua wanafunzi saba huku wengine 64 wakijeruhiwa. Mwaka 2015, jengo jingine la ghorofa sita lilianguka huko Huruma jijini Nairobi na kuua watu sita.

Serikali wakati huo ilianza ukaguzi wa majengo yote hasa ya makazi na ripoti ya ukaguzi ilionyesha kuwa zaidi ya majengo 800 si salama na hivyo yalihitaji kubomolewa kwani hayakidhi viwango vya ubora.

Hata hivyo shughuli hiyo ilisimamishwa baadaye serikali ikidai haikuwa na fedha za kutosha kubomoa majengo yote hayo.

*BBC*

## Pelosi aidhinisha mashtaka dhidi ya Trump kutayarishwa

**WASHINGTON, Marekani**

SPIKA wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi, ametoa ruhusa ya kutayarishwa kwa ibara za mashtaka dhidi ya Rais Donald Trump, hatua muhimu katika mchakato wa kujaribu kumuondoa madarakani kiongozi huyo wa chama cha Republican.

Katika mkutano wake na wanahabari mjini Washington juzi Spika Pelosi alisema atawaomba viongozi wa Bunge kuendelea na mipango ya kutayarisha orodha ya mashtaka dhidi ya Trump ambayo itajumuisha ushahidi uliopatikana kuhusiana na jinsi alivyojishughulisha na suala la Ukraine.

Pelosi alisema matendo ya Trump katika suala la msaada wa ulinzi kwa Ukraine yamekiuka kwa sehemu kubwa misingi ya taifa na kiapo cha ofisi.

"Taarifa zilizopo hazina ubishi, ukweli ni kwamba Trump alitumia madaraka yake vibaya kwa maslahi binafsi na manufaa ya kisiasa kwa kuweka rehani usalama wetu alipozuia msaada wa kijeshi na kutoa nafasi ya mkutano muhimu kwenye ofisi ya rais ili litolewe tangazo la kumchunguza hasimu wake wa kisasia." alisema Pelosi.

Uamuzi wa Pelosi umekuja siku moja baada ya wanazuoni watatu wa masuala ya katiba kuwaarifu wabunge kwamba wanaamini Rais Trump amefanya makosa ya kiwango cha kuweza kushtakiwa na kuondolewa chini ya katiba ya nchi hiyo.

Pelosi alisema Trump amepoteza imani ya umma na kwamba ushahidi uliotolewa hauna shaka kwamba matendo ya kiongozi huyo ni ukiukwaji mkubwa wa imani ya umma na uvunjaji wa kiwango cha juu wa misingi ya katiba.

Trump anatuhumiwa kutumia madaraka yake vibaya kwa kuendesha kampeni iliyowahusisha washirika wake wa ndani ya kuishinikiza Ukraine ipekue uozo dhidi ya mpinzani wake wa kisiasa kutoka chama cha Demcratic, Joe Biden.

Trump anashutumiwa kumtaka rais mpya wa Ukraine Volodymyr Zelensky atangaze kuanzisha uchunguzi dhidi ya mtoto wa Biden, aliyefanya kazi na kampuni ya nishati nchini Ukraine kama sharti la kupatiwa msaada wa ulinzi na kukaribishwa kwa ziara rasmi mjini Washington.

Mashtaka dhidi yake yanaweza kujumuisha matumizi mabaya ya madaraka, rushwa na kuzuia utoaji wa haki.

Trump aliwashambulia wana Democrats akijibu kuwa uamuzi huo wa bunge kwa kusema kupitia ukurasa wa Twitter kuwa wapinzani wake wanataka kumuondoa madarakani bila kuweko sababu ya msingi na kwamba ana matumaini ya kushinda kwa sababu chama chake cha Republican kimeungana vya kutisha dhidi ya mchakato huo.

*DW*

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# Jumba Jekundu-30

**Na Adam Fungamwangwo, (0716 350534)**

Hakuna aliyezungumza kitu kwa dakika tano. Kila mmoja mawazo yaliondoka hapo na kukumbuka mambo mbalimbali nyuma.

"Basi usilie Edina, haya yote ni maisha, na mimi nitakusaidia kadri ya uwezo wangu kuvuka hapa ulipo. Japo mimi sina uwezo wa kipesa, lakini hata wa mawazo tu nitakusaidia."

"Najua najua, Kadili, najua kila kitu. Najua maisha yako, najua familia yako, nachotaka kutoka kwako ni kampani tu, mengine niachie rafiki yangu."

Baada ya kuridhika kukumbatiana, Kadili alirejea kwenye kiti chake na Edina aliendelea kukaa pale alipokuwa awali.

Bado Kadili kuna vitu vilikuwa vinamkereketa. "Niambie Edina, kifo cha mama nacho ni kweli kimetokea kwa sababu ya wewe kumkimbia mume, au maneno tu?"

Alionekana kufikiria kidogo. "Kuna asilimia fulani ya ukweli, kwa sababu mama alifariki siku mbili baada ya mimi kumtoroka mume. Kwanza kabisa mama alikuwa na matatizo ya moyo. Alikuwa na ugonjwa huo kwa muda mrefu na alikuwa anatumia vidonge ambavyo alikuwa akinywa kila baada ya muda fulani au anapohisi hali fulani si nzuri kwenye mwili wake. Nilipofuatilia baadaye niliambiwa kuwa alipata na mshtuko aliposikia mimi nimetoroka kwa mume na kikubwa zaidi ni kwamba sikurudi nyumbani. Na sikurudi kwa makusudi kwa sababu nilikosa ushahidi, mwanzo nilikwambia nilitaka ushahidi niupeleke kwa mama kuwa yule hakuwa mume mwema, lakini nilinyang'anywa ushahidi wa picha za video, unarudije nyumbani, unamwambije mama kuwa nimeondoka kwa mume bila maelezo ya kutosha, hasa ikizingatia kuwa anajua kuwa nimeolewa kwa shinikizo?" Alijibu Edina na kumwangalia kwa makini Kadili kuona kama ameridhika na maelezo yake.

Kadili alionekana si tu kuridhika na majibu yale, lakini pia alionekana kushangaa na kupata habari mpya ambazo zilikuwa zinafanyika nyuma yake tangu alipotolewa kwenye mateso makali kwenye jumba jekundu la kina Edina, chini ya utawala la Madame Pauline, mama mzazi wa Edina ambaye tayari amefariki.

"Ulihudhuria msibani?"

"Ndiyo"

"Hakuwa na tatizo lolote kwa sababu nilidhani, ungeogopa macho ya watu wakiwemo ndugu wa mama yako."

"Kadili, hivi unajua kuwa mimi ndiyo mtoto pekee wa marehemu mama. Kwa hiyo wale wafanyakazi wasingeweza kufanya chochote bila mimi. Mimi ndiye mrithi wake. Jumba lile, majumba mengine, biashara, miradi yake, mali na pesa zote zilizopo nyumbani na benki pia."




"Ndugu zake hawakusema kuwa wewe muuaji, au umesababisha mauaji wenye vikao vya familia?"

Aliangua kicheko cha kike, ghafla akanyamaza.

"Nacheka utafikiri mazuri vile. Kadili siyo kama mimi nafurahia kifo cha mama. Kimeniuma na kimenichoma sana. Nimelia sana kwa sababu mama amenizaa, amenilea na kunisomesha vizuri sana, na pia alikuwa ananipenda mno." alisema na kunyamaza kama mtu anayefikiria kitu hivi.

"Tofauti yetu na mama ni mitazamo tu. Yeye alikuwa na mitazamo yake na mimi mitazamo yangu. Na yote haya yamesababishwa na hayo na sina wa kumlaumu. Na pamoja na haya yote kutokea na kupoteza mama, lakini bado nitabaki na ninachoamini ambacho yeye hakukiamini kamwe. Maana ya hili nitakueleza siku nyingine, lakini tukija kwenye swali lako ni kwamba ndugu wa mama walikuwa wanamfahamu kwa misimamo yake na hata ile harusi ilipokuwa ikifanyika walijua kuwa nimeozeshwa kwa nguvu. Na hata lilipotokea la kutokea, walisikitika na kulia kwa sababu ndugu yao amefariki, lakini walijua ni yeye mwenyewe ndiye alisababisha kwa sababu ya alilazimisha kitu ambacho hakipo.

Nilifika, nikawahi mazishi, nikazika, lakini wakati namtoroka Dk. Kapilima nilikuja kwenye hoteli hii ambayo tumo humu, baada ya siku mbili nikasikia mama amefariki, nikaenda. Nilipomaliza mazishi nikarudi tena hapa."

"Mumeo hakuja kwenye msiba?"

"Aje kufanya nini? Kwanza kitendo cha kunipiga na kuninyang'anya simu yangu nilikwenda kuripoti polisi, kwa hiyo hapo tayari alikuwa yuko katika hatua ya kukamatwa. Kingine nilipofika kwenye msiba mimi ndiyo nilikuwa ndiye mwenye mamlaka kuanzia wakati huo, niliwaambia walinzi akija wamzuie kuingia ndani, labda akae nje, na nadhani hakuja maana angekuja, wale walinzi wangeniambia."

Kadili alishusha pumzi. Tayari alijua kila kitu kilichoendelea. Pamoja na kutambua kuwa alikuwa kwenye hatari ya kukamatwa au kuuawa licha ya kutoka kwenye jumba jekundu, lakini ni Edina ndiyo alikuwa akimfanya awe salama, lakini alitambua kuwa msichana huyo hakuwa na mwanaume mwingine kama alivyokuwa akidhani.

> **"Nacheka utafikiri mazuri vile. Kadili siyo kama mimi nafurahia kifo cha mama. Kimeniuma na kimenichoma sana. Nimelia sana kwa sababu mama amenizaa, amenilea na kunisomesha vizuri sana, na pia alikuwa ananipenda mno." alisema na kunyamaza kama mtu anayefikiria kitu hivi.**

"Nilidhani baada ya kumkimbia Dk. Kapilima utakuwa umekwenda kwa mwanaume mwingine."

Edina aliangua kicheko kikali kikafuatia na sauti tamu iliyosisimua ubongo wa Kadili.

"Wivu huo sasa." Walicheka pamoja.

"Enhee haya yamepita, maisha yako baada kifo cha mama yako yatakuwaje?"

"Sijajua Kadili kama yatakuwa mazuri au mabaya."

"Kwa nini?"

"Kwa sababu itategemea na vitu nilivyopanga kufanya kama vitafanikiwa."

"Nini ambacho umepanga bibie?"

"Kwanza nikimaliza kukaa hapa hotelini ambako nimeamua kuishi ili nipate utulivu wa kutosha, nirudi nyumbani, nifungue mirathi, kila kitu cha mama kiwe kwenye mikono yangu, hadi lile kundi la wafanyakazi wawe chini ya himaya yangu. Nichambue biashara gani za mama ambazo nitaweza kuendelea kuziendesha na zipi ambazo zisiwezi niachane nazo."

"Vizuri hilo ni muhimu sana."

"Ila nina ombi moja."

"Omba tu."

"Haya yote siwezi kufanya peke yangu bila ya kuwa na mtu wa kunisaidia, hivyo naomba msaada wako ili tusaidiane. Unajua kuna maeneo nikienda mimi kama mwanamke inakuwa kero kidogo, lakini kama kukiwa na mwanaume kunakuwa na unafuu."

"Siwezi kukupinga hata kidogo Edina, umefanya mambo mengi juu yangu na mimi sasa ni wakati mzuri wa kuonyesha mrejesho wa kile ulichonitendea kuulinda uhai wangu."

"Usijali Kadili wewe ni rafiki yangu, swahiba yangu, nimeutetea uhai wako kwa gharama zote kwasababu wewe kwangu ni mtu muhimu mno."

"Ndiyo maana nikasema kuwa nitafanya chochote kile, hata kama ukitaka nisimame juu ya bahari. Kwa sababu hapa nitakachofanya ni kulipa tu wema ulionifanyia ambao utakuwa ni wa kuiga tu. Wewe wa kwako Edina ni wa asili kwa sababu ulianza mwanzo bila kutegemea malipo au wema kutoka kwangu kwa hiyo wema wa asili na wa kuiga hatolingana kamwe."

Maneno hayo yalimchoma Edina, alinyanyuka taratibu na kumfuata Kadili. akamkumbatia. Ilionekana kabisa hawa wote wawili wana kitu ndani ya mioyo yao ambayo hawataki kuweka wazi.

Kadili ndani ya moyo wake alikuwa anampenda Edina, lakini ufukara na woga ndiyo uliomfanya ashindwe kabisa kumwambia neno 'Nakupenda'. Tangu alipokutana naye kwa mara ya kwanza 'blue star' kule Sinza hadi muda huo anakumbatiwa na mtoto huyo mkali wa kitajiri, mwenye uzuri usiomithilika, Kadili alikuwa akifa na kidonda cha roho.

Pamoja na wema wote aliomtendea na kuonekana kumjali hadi muda huo, Kadili bado alikuwa hajui ndani ya moyo wa Edina alikuwa akifikiria nini. Alifanya hivyo kwa sababu tu ya kumuonea huruma kutokana na matatizo yote aliyasababisha yeye, au Edina alikuwa na lake moyoni?

*Itaendelea Jumamosi*

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**WILLY FADHILI NGOYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 542 AZF** AINA YA **FUSO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/JNI/RB/538285/2019.**

115548002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BEATRICE DEO MMARY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 861 CML AINA YA FUSO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/JNI/RB/538305/2019.**

115548102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**FORM II**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 88/2019**

**OMBI LA NURU HASSAN BAKARI KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU HADIJA MWATATU SALUM KISAMA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

WATU WOTE WANAODAI KUWA NA MAHUSIANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO WANAALIKWA KUJA NA KUHUDHURIA KESI WAKITAKA MNAMO TAREHE 17-12-2019 KABLA YA MUOMBAJI KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO.

WOSIA WA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA. TRH 06/12/2019

PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

Sahihi ya Hakimu.

115547479

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**FORM II**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 84/2019**

**OMBI LA ZILIPA STANLEY LUSINDE KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU MAGRETH STANLEY MASIMBA**

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA
WATU WOTE WANAODAI KUWA NA MAHUSIANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO WANAALIKWA KUJA NA KUHUDHURIA KESI WAKITAKA MNAMO TAREHE 16-12-2019 KABLA YA MUOMBAJI KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO.

WOSIA WA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA. TRH 06/12/2019

PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

Sahihi ya Hakimu.

115547802

## MASHINE INAUZWA



Mashine ya matofali ya umeme inauzwa (made in Sweden). Inatengeneza matofali ya aina 4:

Matofali ya kawaida (inchi 6), Matofali ya kawaida (inchi 9), Matofali yenye shimo (holo bricks) na pavement blocks. Tunapatikana Undali street, Block 185 near Diamond Jubilee.

**Mawasiliano:**
**0711 506758, 0787 446505.**

115547702

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SCHMEICHEL:

## SOLSKJAER BADO HAYUPO SALAMA



**MANCHESTER, England**

PETER Schmeichel amesema ushindi wa Manchester United dhidi ya Tottenham Hotspurs hausaidi kitu na kwamba kocha Ole Gunnar Solskjaer ataendelea kuwa na presha.

Schmeichel ambaye ni golikipa wa zamani wa klabu hiyo amebainisha kuwa kibarua cha Solskjaer bado hakipo salama licha ya timu yake kucheza vizuri na kushinda 2-1 dhidi ya Hotspur kwenye Ligi Kuu England, Jumatano.

Mabao mawili ya Marcus Rashford yaliisaidia Man United kuibuka na ushindi kwenye mchezo huo wakimwaadhibu kocha wao wa zamani, Jose Mourinho, ambaye kwa sasa anainoa Spurs.

Baada ya matokeo ya ovyo mfululizo jambo hilo lilimfanya Solskjaer kuwa kwenye presha kubwa ya kupoteza ajira yake huku kocha wa zamani wa Spurs, Mauricio Pochettino akihusishwa na miamba hiyo ya Old Trafford na kama angepoteza dhidi ya Spurs basi hali ingekuwa mbaya zaidi kwa upande wake.

Hata hivyo, Schmeichel anaamini kwamba matokeo ya juzi hayawezi kumweka salama Solskjaer, akisema: "Matokeo yatampa amani ya siku chache tu, lakini furaha yake itaisha kwenye mechi ijayo akipoteza. Ana timu changa sana na tusisahau kwamba amekuwa kwenye hali mbaya kwenye timu hiyo."

Schmeichel amekiri kwamba alikuwa kwenye wasiwasi mkubwa akitazama Man United ikicheza na timu inayonolewa na Mourinho, lakini alisema alivutiwa na kiwango cha timu yake ya zamani hasa baada ya kutuliza akili yao na kusaka ushindi kufuatia bao la kusawazisha la Dele Alli, kwamba halikuwavuruga.

Ushindi huo uliwaondoa Man United kwenye nafasi ya 10 na kupanda juu kidogo lakini leo, Jumamosi watakuwa na shughuli pevu kwa kuwakabili Manchester City pale katika Uwanja wa Etihad.

## PSG WATAKA VINICIUS AWE CHAMBO YA MBAPPE REAL

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain wameripotiwa kwamba wanamtaka Vinicius Junior wa Real Madrid na kwamba ajumuishwe kwenye ofa yao ya kumsajili Kylian Mbappe wakati dirisha la uhamisho wa majira ya joto mwakani.

Mbappe kwa sasa yupo katika msimu wake wa tatu huko PSG na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuachana na timu hiyo mwishoni mwa msimu huu wa 2019-20.

Kwa muda mrefu mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa amekuwa akihusishwa na Real Madrid, ambapo Kocha Zinedine Zidane anahaha usiku na mchana akajiunge na timu yake.

Kwa mujibu wa Gazeti la AS, miamba hiyo ya La Liga imeambiwa kama inamtaka Mbappe, basi ni lazima wamjumuishe Vinicius kwenye ofa yao.

Mkurugenzi wa soka wa PSG, Leonardo amekuwa akimfuatilia Vinicius, aliyenaswa na 'Los Blancos' hao akitokea Flamengo kwa pauni milioni 40 mwaka jana.




## INTER WAMNYATIA AUBAMEYANG

**MILAN, Italia**



KLABU ya Inter Milan imeripotiwa kumnyatia nahodha wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang.

Inter Milan wanataka saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon baada ya kuibuka kwa uvumi kwamba staa huyo anaweza kuachana na Arsenal wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Aubameyang kwa sasa ameanza kufikiria upya hatima yake Arsenal baada ya kuona mambo hayaendi wakiwa nyuma kwa pointi saba kuikamata nafasi ya nne Ligi Kuu England ambayo inatoa tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwenye uhamisho wa dirisha lililopita majira ya kiangazi, mshambuliaji huyo alikuwa akihusishwa na vigogo wa Hispania, Barcelona na Real Madrid, lakini sasa Inter wanaonekana kuwa siriazi kuitaka saini yake ili akajiunge na timu yao dirisha la uhamisho wa Januari litakapofunguliwa.

Kocha wa Inter Milan, Antonio Conte anataka huduma ya Aubameyang katika dirisha hilo baada ya kuwa na wasiwasi huenda akampoteza mshambuliaji wake Lautaro Martinez, anayesakwa kwa nguvu zote na Barcelona.

## HABARI MICHEZO




# SCHOLES

## AMKATAA LJUNGBERG ARSENAL

**LONDON, England**

NYOTA wa zamani wa klabu ya Manchester United, Paul Scholes, amesema Freddie Ljungberg hana uwezo wa kuivusha Arsenal.

Ljungberg mchezaji wa zamani wa Arsenal alipewa mikoba ya kuinoa klabu hiyo kwa muda baada ya kufukuzwa kwa Unai Emery pale kwenye dimba la Emirates.

Arsenal ilitoka sare ya mabao 2-2 na Norwich City katika mechi yao ya kwanza tangu walipomfuta kazi aliyekuwa kocha wao Mhispaniola, Emery kabla ya juzi usiku kuchapwa 2-1 dhidi ya Brighton & Hove Albion katika Uwanja wa Emirates.

"Ungemtarajia kumwona akiwa kwenye vazi la suti safi inayoendana na kazi yake kwa sasa. Mimi naona alianza vizuri kwa matokeo, lakini kuacha kuvaa suti na tai, huo ni ukosefu mkubwa wa nidhamu," alisema Scholes na kuongeza.

"Sidhani kama yeye ni mtu sahihi kwenye kazi hiyo."

Lakini, maneno hayo ya Scholes yanaweza kuwa kama kumpigia muziki tu mbuzi kwa sababu Ljungberg anachodai yeye hajioni kuwa ni kocha wa kudumu katika kikosi hicho cha Arsenal.

Sasa kitendo cha Kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers kuwafungulia mlango Arsenal kama wanamtaka kinathibitisha wazi Ljungberg hatakuwa na muda mrefu wa kuendelea kukalia kiti cha ubosi huko kwenye kikosi hicho cha Emirates.

Ljungberg, ambaye alikuwamo kwenye kile kikosi cha Arsenal kilichocheza kwa msimu mzima bila ya kupoteza, alisema:

"Ni heshima kubwa. Nataka kufanya vizuri kwa kadri ninavyoweza kwenye klabu hii bora. Najisikia furaha na nataka nifanye kazi nzuri zaidi.

"Nipo hapa kuisaidia klabu kwa kadri niwezavyo, kurudisha ari klabuni na kwa mashabiki. Kama tutacheza soka zuri na kupata matokeo mazuri, hakutakuwa na kitu kingine cha kufanya kurudisha ari. Nina uhakika wa kufanya hilo, la sivyo singekubali kazi hii nilipoombwa kufanya hivyo."

# Bale adaiwa kutaka kurudi Tottenham

**LONDON, England**


GARETH Bale ameripotiwa kwamba huenda anataka kurudi kwenye klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur baada ya kusifia timu hiyo kwa uamuzi wa kumchukua kocha Jose Mourinho.

Mourinho alichaguliwa kuwa kocha wa Spurs wiki mbili zilizopita baada ya Mauricio Pochettino kufutwa kazi kufuatia kuinoa timu hiyo kwa kipindi cha miaka mitano.

"Kuwa na Jose Mourinho kwenye timu huo ni ujumbe maalumu kutoka kwa timu, nadhani ni kocha wa ushindi," alisema Bale.

"Tottenham wanataka kushinda mataji na sidhani kama kutakuwa na muunganiko mzuri zaidi ya Mourinho na Tottenham wakijaribu kuwa pamoja kubeba mataji."

Kutokana na hilo watu wamekuwa wakiamini kwamba kuna uwezekano Bale akafungua milango ya kurudi Spurs hasa kwa kipindi hiki mambo yake yakiwa magumu pale Real Madrid, ambako hakubaliki sana.



# Klopp ampigia hesabu Sancho

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Liverpool, Jurgen Klopp, amegoma kufuta mpango wake wa kumsajili Jadon Sancho na kufichua dili hilo linaweza kufanyika dirisha la Januari.

Liverpool imekuwa ikihusishwa na mpango wa kumsajili kinda huyo wa Kingereza baada ya ripoti kudai kwa sasa hana furaha huko Borussia Dortmund.

Klopp amekiri anamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, kwa sababu anaamini ni bora na amekuwa akifanya mambo mazuri ndani ya uwanja.

Saini yake pia inawindwa na klabu kadhaa ikiwamo Manchester United na Manchester City, ambayo aliwahi kuitumikia huko nyuma na kuna kipengele kwenye mkataba wake kinachodai Dortmund hawatamruhusu aondoke kabla ya kuwahusisha Man City kwanza na kama watashindwa bei ndipo hapo timu nyingine zinazomtaka zitambeba.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD PIGO REAL, KUIKOSA EL CLASICO

●●●Marcelo pia hatarini kuikosa Barca kutokana na majeraha ya kigimbi cha mguu, huku...

**MADRID, Hispania**

Eden Hazard ataikosa El Clasico [dhidi ya Barcelona] Desemba 18, mwaka huu baada ya Real Madrid kuthibitisha anasumbuliwa na majeraha ya kifundo cha mguu, 'enka'.

Hazard alilazimika kutoka nje wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain mwishoni mwa mwezi uliopita na alihitaji msaada wakati wa kutoka uwanjani.

Kocha Zinedine Zidane alionyesha wasiwasi baada ya mechi, akiamini ni "zaidi ya pigo rahisi", kwa vipimo vya mwanzo akidai Hazard alikuwa akisumbuliwa michubuko tu.

Lakini vyombo vya habari vimeripoti wasiwasi umeongezeka kwa hali ya Hazard kufuatia kuhitaji msaada wa magongo ili kuweza kutembea.

Madrid baadaye ilimpeleka Hazard kwenye vipimo zaidi na kugundua kuwa kwa mpasuko kidogo katika enka.

Wakati klabu hiyo ikiwa bado haijathibitisha ni kwa muda gani atarajia atakuwa nje ya uwanja, majeraha kama hayo huchukua takriban mwezi mmoja kupona, na taarifa za vyombo vya habari zinaeleza kuwa Hazard ataukosa mchezo wa El Clasico.

Madrid inatarajia kuivaa Barca katika Uwanja wa Camp Nou Desemba 18, tarehe hiyo ikiwa imepangwa upya baada ya awali mechi hiyo kutarajiwa kupigwa Oktoba 26, mwaka huu na kuahirishwa kutokana na machafuko ya kisiasa Catalunya.

Marcelo pia anahofiwa kuikosa mechi hiyo baada ya Madrid kuthibitisha kuwa anasumbuliwa na majeraha ya kigimbi cha mguu.

Wakati majeraha yake yakidhaniwa kutokuwa makubwa kama Hazard, gazeti linalochapa zaidi taarifa za Madrid, Marca limedai kuwa atakuwa nje kwa wiki tatu.

Madrid na Barca zinafungana pointi kila moja ikiwa na alama 31 kutokana na mechi 14 kwenye msimamo wa La-Liga, pointi moja mbele dhidi ya Sevilla inayonolewa na kocha wa zamani wa 'Blancos' hao, Julen Lopetegui, ambao wameshuka dimbani mara 15.

Kuelekea El Clasico, Madrid itaivaa Espanyol na Valencia katika Ligi Kuu, wakati pia itavaana kwanza na Club Brugge kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya mchezo huo dhidi ya Barca.

## KWA UFUPI

**SUAREZ AMTETEA MESSI**
Maoni ya wazi ya Lionel Messi kuhusu kustaafu "hayakueleweka", kwa mujibu wa mchezaji mwenza wa Barcelona, Luis Suarez. ***(Livescore)***

**LEICESTER, RODGERS WAJIFUNGIA**
Leicester City imefungua mazungumzo na kocha wake, Brendan Rodgers kuhusu mkataba mpya mnono lengo likiwa ni kumzuia kujiunga na Arsenal.***(Telegraph)***

**PEREIRA ANUKIA EVERTON**
KOCHA wa Shanghai SIPG, Vitor Pereira ni mmoja wa wanaowaniwa kurithi mikoba ya Marco Silva aliyetimuliwa Everton. ***(Mail)***

**POCHETTINO BASI TENA BAYERN**
KOCHA wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino hatakuwa kocha wa Bayern Munich. ***(Bild - in German)***

**FATI AJIFUNGA UPYA BARCA**
MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ansu Fati, 17, amesaini mkataba mpya wenye kipengele kinachomruhusu kuuvunja kwa dau ambalo litaongezeka hadi kufikia pauni milioni 337.5 wakati atakapokuwa mchezaji wa kikosi cha kwanza. ***(FC Barcelona)***

**ALLEGRI AJINOA KUTUA EPL**
KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri, amesema haturudi katika kazi hiyo hadi majira ya joto lakini amekuwa akijifunza Kingereza wakati huu akihusishwa na kufanya kazi Ligi Kuu England. ***(ESPN)***

**GUARDIOLA KUMREJESHA TORRENT**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anaweza kumrejesha Domenec Torrent kama msaidizi wake endapo Mikel Arteta ataondoka na kwenda kuinoa Arsenal. ***(Sun)***

**ERIKSEN BADO LULU UNITED**
Manchester United bado inatumai kumsajili kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, 27, katika dirisha la Januari baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Denmark kuikataa majira ya joto. ***(Mirror)***

**HAALAND KUNUNULIKA JANUARI**
MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg na Norway, Erling Braut Haaland, 19, anaruhusiwa kuvunja makataba wake Januari kwa pauni milioni 17. ***(Manchester Evening News via Bild)***

**ZAHA AWINDWA CHELSEA**
Chelsea inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, 27, majira yajayo ya joto. ***(Independent)***

**SANCHO AZUIWA DORTMUND**
Borussia Dortmund inataka kuendelea kumbakiza mshambuliaji wa England, Jadon Sancho, 19, hadi mwishoni mwa msimu. ***(Telegraph)***

**WACHEZAJI WAMPIGANIA SOLSKJAER**
KABLA ya kuibuka na ushindi dhidi ya Tottenham katikati ya wiki, wachezaji wa Manchester United, waliuambia uongozi wa klabu hiyo usimtimue kocha Ole Gunnar Solskjaer. ***(Times)***

**GIROUD AKOMALIA KUONDOKA**
MSHAMBULIAJI asiyepewa nafasi Chelsea, Olivier Giroud, 33, kuna uwezekano wa kuondoka Januari na klabu hiyo ikitaka asubiri hadi majira ya joto aondoke akiwa huru. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

# MALALE ARITHI MIKOBA YA MATOLA POLISI TANZANIA

**Na Focus Nicus**

BAADA ya Klabu ya Simba kumalizana rasmi na Kocha wa Polisi Tanzania, Selemani Matola, hatimaye timu hiyo ya 'walinda usalama' wa nchi, yenye makao yake mkoani Kilimanjaro, imemtangaza Malale Hamsini kurithi mikoba ya kiungo huyo wa zamani wa Taifa Stars aliyetua kuwanoa 'Wekundu wa Msimbazi..

Malale ambaye alitemeshwa mzigo na Ndanda FC kwa kile kilichoelezwa ni kutokana na mwenendo mbaya wa timu hiyo, ametangazwa rasmi jana kurithi mikoba ya Matola.

Utambulisho wa Malale ulifanyika jijini Dar es Salaam jana chini ya Mwenyekiti wa timu ya Polisi Tanzania, Kamishna Charles Mkumbo.

Malale sasa ana nafasi ya kudhihirisha ubora wake na kuonyesha Ndanda ilifanya makosa kumtimua, kwa kuhakikisha anaitoa Polisi Tanzania kutoka nafasi ya 13 iliyopo kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kushuka dimbani mara 11 na kuvuna pointi 16.

Katika mechi hizo, Matola aliiongoza Polisi Tanzania kushinda mechi tano na kupoteza tano huku ikitoka sare mchezo mmoja.

Hata hivyo, Malale atapaswa kutumia vema dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 16, mwaka huu, kuimarisha safu ya ulinzi ya kikosi hicho kwani imeonekana kuvurunda zaidi kufuatia kuruhusu mabao 11 yakiwa ni sawa na idadi ya yaliyofungwa na safu ya ushambuliaji ya timu hiyo.

TUNAWEZA...



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya walemavu wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam FC: Hatutaingia sokoni dirisha dogo

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 16, mwaka huu hadi hapo Januari 15, mwakani, benchi la ufundi la Azam FC limesema halina mpango wa kusajili au kutema mchezaji yeyote katika kikosi chao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Idd Cheche, alisema wachezaji wao wote wana viwango vizuri na hawaoni pengo lolote linalohitaji kuboreshwa katika dirisha hilo.

Alisema kwa sasa kikosi chao kinaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya Ligi Kuu pamoja na mchezo wa Kombe la Shirikisho (FA Cup) dhidi ya African Lyon.

"Hatuna mpango wa kusajili mchezaji yeyote katika usajili wa dirisha dogo, wachezaji wetu wote wana uwezo mkubwa," alisema Idd.

Aidha, aliahidi timu hiyo kufanya vizuri msimu huu wa Ligi Kuu kwa kuendelea kutoa ushindani kwenye ligi hiyo ambayo wapo nafasi ya tatu wakiwa pointi tano nyuma ya vinara Simba waliopo kileleni na pointi zao 25 wakifukuziwa na Kagera Sugar yenye alama 24 katika nafasi ya pili.

Hata hivyo, Simba na Azam zenyewe zimeshuka dimbani mara 10 wakati Kagera Sugar pointi zake zikitokana na mechi 13 ilizocheza hadi sasa wakati huu ligi hiyo ikiwa imesimama kupisha michuano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati inayotarajiwa kuanza leo nchini Uganda hadi Desemba 20.

# Minziro ataka 12 wapya Pamba FC

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA mtaalamu wa kupandisha timu Ligi Kuu, Felix Minziro, amemwaga mkakati wake wa usajili ili kuipandisha Pamba FC Ligi Kuu Bara.

Minziro ambaye kwa sasa ni kocha mkuu wa Pamba FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, anaongoza kwa rekodi nzuri nchini ya kuzipandisha timu kucheza Ligi Kuu Bara na kutimuliwa baada ya kukamilisha lengo hilo.

Makocha wengine nchini wenye rekodi nzuri ya kupandisha timu Ligi Kuu ni pamoja na Hassan Banyayi na Bakari Shime ambaye kwa sasa anainoa timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars.

Kuelekea usajili wa dirisha dogo Desemba 16, mwaka huu, Minziro amesema anataka kusajili wachezaji zaidi ya 12 ili kuboresha kikosi chake.

Miongoni mwa timu Minziro alizozipandisha Ligi Kuu na kupigwa chini ni Ruvu Shooting, Singida United na KMC FC.

"Mpango wangu ni kusajili wachezaji zaidi ya 12 wenye uwezo mkubwa ambao watafanya kazi ya kutafuta matokeo chanya ndani ya kikosi chetu, ushindani ni mkubwa na tayari nimeeleza haya yote kwenye ripoti," alisema.

Kwa upande wake Kaimu Katibu wa Pamba FC, Johnson James amethibitisha kupokea ripoti hiyo na kuahidi uongozi kuifanyia kazi kwa ukaribu.

"Ni kweli kocha ameleta ripoti kwa sasa kinachofanyika ni kuitazama na kuifanyia kazi, malengo yetu ni kushiriki Ligi Kuu Bara na ili tufanikiwe lazima tuwe na kikosi imara,"

# WASAGA FC YAJIVUNIA NYOTA LIGI KUU BARA

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa Musoma**

TIMU ya soka ya Wasaga FC ya Kijiji cha Kasoma Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, imejivunia kutoa wachezaji watatu, ambao kwa sasa wako katika timu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara.

Wasaga FC ni miongoni mwa timu zinazojiandaa kushiriki Ligi Daraja la Tatu ngazi ya mkoa, huku ikisubiri kuchukua fomu kwa ajili ya kukamilisha usajili wa wachezaji wake, kabla ya Desemba 15, mwaka huu.

Katibu wa timu hiyo, Mneji Marobe, aliwataja wachezaji ambao wametoka Wasaga FC na kwenda timu za Ligi Kuu kuwa ni Kauswa Manumbu aliyesajiliwa na Biashara United kabla ya kutua Mbao FC.

"Wengine ni Sixtus Sabilo aliyeanzia Stand United, KMC na sasa yupo Polisi Tanzania na yupo pia Omary Juma, ambaye anaichezea Biashara United," alisema Marobe.

Marobe alisema, anaamini wachezaji hao huko waliko watakuwa mabalozi wazuri kuitangaza vema timu yao hiyo, na uhakika inaweza kufika mbali baada ya kufanikiwa kutinga ligi hiyo ngazi ya mkoa.

Aidha, katibu huyo amemuomba Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo kuwa mmoja wa wafadhili wa timu hiyo ili kuisaidia kwa hali na mali ili iendelee kusonga mbele.

"Tumemuomba mbunge wetu huyo, kwani timu iko kwenye jimbo lake, na ameshauri tumpe kwanza muda ili atafakari jinsi ambavyo ataweza kutusaidia na kuhakikisha Wasaga FC inasonga mbele," alisema.

# Michezo

Jumamosi Desemba 7, 2019

Nipashe




## Hazard pigo Real, kuikosa El Clasico

HABARI UK 30

PAMBANA...



Kipa wa Arsenal, Bernd Leno, akipambana kuucheza mpira dhidi ya mshambuliaji wa Brighton, Neal Maupay, aliyeifungia timu yake bao la ushindi dakika ya 80 wakati wakishinda 2-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi. Aliyesimama akishangaa badala ya kumsaidia Leno ni kiungo Granit Xhaka. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA KUANDIKA REKODI MPYA LEO

●●● Jiji kuzizima wakizindua viwanja vya Bunju, waja na 'One Team, One Dream, Bunju 2019', huku...

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya miaka 83 tangu ianzishwe mwaka 1936, Klabu ya Simba leo itaandika rekodi mpya kwa kuuzindua rasmi Uwanja wao wa Bunju kwa kuutambulisha kwa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kabla ya kufanyika kwa mkutano mkuu jijini Dar es Salaam kesho.

Simba imekamilisha ujenzi wa viwanja viwili vya mazoezi, wa nyasi bandia na nyasi asili vilivyopo Bunju jijijini Dar es Salaam na timu hiyo inatarajiwa kuanza kufanya mazoezi katika viwanja hivyo baada ya kutambulishwa kwa mashabiki na wanachama wa klabu hiyo leo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mwina Kaduguda alisema leo kutakuwa na jambo kubwa ambalo litaacha historia nchini.

"Leo tutakuwa na jambo kubwa la uwanja, tunaomba mashabiki na wanachama wetu waje kushuhudia uwanja huo pale Bunju," alisema Kaduguda.

Aidha, alisema anaamini uwanja huo utazidi kuipa mafanikio timu hiyo ambayo mpaka sasa inashikilia usukani wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 25 baada ya mechi 10.

**Kwa upande wake Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara alisema: "Jumamosi wanachama na mashabiki tutatembelea uwanja wetu wa Bunju baada ya mradi wa ujenzi wa awamu ya kwanza kumalizika. Usipange kukosa."**

Na kuelekea shughuli hiyo kubwa ya kihistoria katika klabu hiyo, Simba imeandaa jezi maalum zilizoandikwa "One Team, One Dream, BUNJU 2019", ambazo kwa kila shabiki anayehitaji ametakiwa kutembelea ukurasa wa Instagram wa klabu hiyo ili kupata maelekezo namna ya kuzipata.

Baada ya ujezi huo kukamilika chini ya Mwekezaji wao, Mohamed "Mo" Dewji, Simba pia imeeleza sasa kuhamia katika mpango wa kujenga hosteli kwa ajili ya timu hiyo ya wakubwa na ile ya vijana.

Hiyo ni hatua kubwa kwa klabu hiyo kufikia, ambayo sasa inawaacha watani zao wa jadi, Yanga iliyoanzishwa mwaka 1935 ikiwa klabu kongwe inayoendelea kukodi uwanja wa mazoezi.

Kwa upande wa mkutano mkuu, Kaduguda alisema utafanyika kesho kwenye Ukumbi wa Mwalimu Nyerere, na kufafanua kuwa anaamini kila kitu kitakwenda sawa kutokana na maandalizi yote kukamilika asilimia 100.

"Kesho tunatarajia kufanya mkutano wetu mkuu maandalizi mpaka sasa yamekamilika tusubiri kuona na kusikia vitakavyojadiliwa," alisema Mwenyekiti huyo ambaye kitaaluma ni mwalimu na kocha.

## Kili Stars, Zanzibar kesho, Uganda leo

**Na Somoe Ng'itu, KAMPALA**

PAZIA la mashindano ya Kombe la Chalenji mwaka huu linatarajiwa kufunguliwa leo kwa wenyeji, timu ya soka ya Taifa ya Uganda (Cranes), kuwakaribisha Burundi katika mechi ya ufunguzi ya mashindano hayo itakayopigwa kwenye Uwanja wa Namboole ulioko jijini hapa.

Mechi hiyo itatanguliwa na mchezo mwingine kati ya Djibouti dhidi ya Somalia, utakaochezwa kwenye uwanja huo huo, kuanzia saa nane mchana.

Miamba ya Tanzania Kilimanjaro Stars na Zanzibar Heroes yenyewe itashuka dimbani kesho kuzivaa Harambee Stars ya Kenya na Sudan.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye, alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika na anaamini timu zote zitaonyesha ushindani katika michuano hiyo.

Musonye alisema anaamini michuano hiyo itawasaidia wawakilishi wa Cecafa ambao wamekata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa ndani (CHAN), kujiandaa na mashindano hayo yatakayofanyika Aprili mwakani.

"Tuko tayari kwa mashindano, tunaamini kila timu imekuja hapa kushindana, mashindano haya ni sehemu nyingine ya kutangaza vipaji vya wachezaji wa ukanda huu, wengi wamepita hapa na sasa wanacheza Ulaya, " alisema Musonye.

Alisema kuwa timu mbili zitakazofanya vizuri kutoka katika kila kundi, zitatinga hatua ya fainali ya mashindano hayo yanayotarajiwa kumalizika Desemba 19, mwaka huu.

Naye Kaimu Rais wa Chama cha Soka Uganda (Fufa), Justus Mugisha, alisema anawatakia wageni wote kuwa na wakati mzuri kuanzia siku ya kwanza hadi ya mwisho ya michuano hii.

"Kama wenyeji tunaamini mambo yatakwenda vizuri, kila timu imekuja kupambana, kusaka matokeo chanya, tunaamini tutashuhudia michuano yenye ubora," alisema Mugisha.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >